




UKURASA 4

**MWILI** wa Prof. Ngowi, dereva kuagwa leo Dar




# Nipashe

Alhamisi Machi 31, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580901

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11



UKURASA 4

## UMMY AKIRI HUDUMA MBOVU KATIKA HOSPITALI ZA SERIKALI

# MAZITO

**RIPOTI** CAG, TAKUKURU zaibua madudu, Rais atangaza MSD kufumuliwa, ukaguzi magari kufanywa nje... *Endelea Uk. 2, 3 & 19*



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2020/2021 kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Basi lililoua Moro ladaiwa kutengenezwa kwa vifaa vya ujenzi

UKURASA 4

**MICHEZO** **MAYELE AMPA PRESHA LUSAJO** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea taarifa ya Taasisi ya TAKUKURU kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, CP Salum Hamduni, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Mazito ripoti za CAG na TAKUKURU

**Na Sanula Athanas**

MAZITO Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na kuwasilishwa kwa Rais taarifa za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21.

Baada ya kukabidhiwa ripoti hizo Ikulu mkoani Dodoma jana, Rais Samia Suluhu Hassan aliweka wazi atafanya mabadiliko ya uongozi katika taasisi zilizobainika kuwa na utendaji mbovu.

Ripoti ya TAKUKURU ilibainisha kuwapo kwa viashiria vya ubadhirifu katika utekelezaji wa miradi 222 inayogharimu zaidi ya Sh. bilioni 79, huku CAG akianika dosari kwenye taasisi na mashirika mbalimbali ya umma.

Vilevile, safari hii CAG amekuja na taarifa ya ukaguzi kuhusu fedha zinazokusanywa kutokana na mabadiliko ya sheria yaliyoruhusu washukiwa wa makosa mbalimbali ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha kukiri kosa na kuingia makubaliano maalumu na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kulipa fedha.

Katika hilo, CAG pia amekagua fedha na mali zilizotaifishwa kutokana na utaratibu huo mpya katika mwenendo wa kesi za jinai.

Ikirejewa Aprili mwaka jana, wadau kadhaa wakiongozwa na Chama cha ACT-Wazalendo walipaza sauti, wakitaka kufanyike ukaguzi na ikiwezekana kuwekwa wazi kwa taarifa kuhusu kiasi cha fedha kilichokusanywa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kutoka kwa watuhumiwa wa makosa ya jinai waliokiri makosa na kukubali kulipa.

Kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Tanzania, CAG, Charles Kichere, jana aliwasilisha kwa Rais ripoti 12, zikijumuisha ukaguzi wa hesabu za serikali za mitaa, serikali kuu, mashirika ya umma, ufanisi na ukaguzi maalumu.

Kuhusu agizo la Rais la Oktoba 10, mwaka jana la kufanya ukaguzi maalumu wa matumizi ya fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19, CAG alisema anaendelea na ukaguzi huo na pindi akikamilisha kazi ripoti itatua kwa Rais na itawekwa wazi kwa umma.

Miongoni mwa maeneo yaliyobainika kuwa na dosari ni utendaji wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ambayo Rais Samia alitangaza inahitaji mabadiliko makubwa; upungufu katika upakuaji wa shehena za mizigo bandarini; na ukaguzi wa magari yanayonunuliwa nje ya nchi, Rais Samia akiagiza yawe yanakaguliwa nje badala ya utaratibu wa sasa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kufanya kazi hiyo.

Mashirika na taasisi zingine za umma zilizobainika kuwa na dosari ni pamoja na Taasisi ya Mifupa na Mifupa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Shirika la Mawasiliano (TTCL), Shirika la Masoko Kariakoo, Shirika la Reli (TRC) na mamlaka za maji.

Ukaguzi wa CAG pia umebaini dosari kwenye hesabu za vyama vya siasa, CUF, ADC, SAU na UDP vikiwa sehemu ya vyenye upungufu.

CAG Kichere pia alibainisha kuwapo upungufu katika ulipaji wa mafao nchini kutokana na taasisi za umma kutowasilisha kwa wakati michango ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) huku taasisi 10 za serikali zikilimbikiza deni la zaidi ya Sh. trilioni 1.17 kwenye Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) tangu mwaka 2007 zilipokopeshwa.

Ripoti ya CAG ina taarifa za ukaguzi kuhusu utekelezaji wa miradi ya kimkakati, akianika kuwapo kwa dosari nyingi, huku jicho lake pia likibaini udhaifu katika huduma za Shirika la Umeme (TANESCO) katika kuwaunganishia huduma wateja.

Hii ni ripoti ya tatu ya mwaka kuwasilishwa na CAG Kichere tangu alipoteuliwa Novemba 3, 2019, akichukua nafasi ya mtangulizi wake, Prof. Mussa Assad.

## Bohari Dawa kusukwa upya

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Bohari Kuu ya Dawa (MSD), inahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa ikiwamo kufumua uongozi mzima kwa lengo la kuleta ufanisi katika utendaji kazi.

Amesema hatua hiyo inatokana na utendaji taasisi hiyo kutoridhisha ikiwamo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Akizungumza jana baada ya kukabidhiwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Rais alisema MSD ilifanikiwa kupata soko la dawa kwenye nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) lakini ikashindwa kukidhi mahitaji.

Sambamba na soko hilo, Rais Samia alisema pia imeshindwa kutosheleza hata mahitaji ya ndani ya nchi.

"MSD inahitaji kufanyiwa 'overhauling' (kusukwa upya) kuanzia uongozi wa juu, ununuzi, vitengo vyote. Katibu Mkuu Kiongozi hili linahitajika kama tulivyofanya TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania). Nasema hivi kwa sababu MSD ilikuwa inapata 'tender' (zabuni) kugawa au kuuza dawa ndani ya SADC.

"Hatua tuliyofika leo hata ndani watu wanalalamika tutauzaje huko SADC. Bado SADC wana imani na Tanzania wanataka kuipa 'tender' MSD. Tuirekebishe isimame yenyewe na kufanya kazi," alisema Rais Samia.

Rais pia alisema yako maombi mengi ya uwekezaji wa viwanda vya dawa yanayowasilishwa serikalini kutoka watu binasi sababu kubwa ikiwamo uwapo wa soko la bidhaa hizo.

"Tumepokea maombi ya uwekezaji wa viwanda vya dawa kawa sababu soko ni EAC (Jumuiya ya Afrika Mashariki) na SADC. Lakini tukiwa na MSD aina hii inayosuasua namna hii hatuwezi kwenda," alisema.

# CAG aibua madudu katika miradi kimkakati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, ameibua madudu katika miradi ya kimkakati ikiwamo kuchelewa kwa ujenzi wa bwawa la kufua umeme wa maji la Mwalimu Julius Nyerere kwa asilimia 46.45.

Kichere alibainisha hayo jana Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma alipokuwa akiwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021 kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Hadi kufikia Oktoba 2021 mradi ulipangwa kukamilika kwa asilimia 94.47, hata hivyo nilibaini kuwa mradi ulikamilika kwa asilimia 48.02 ukiwa umechelewa kwa asilimia 46.45,"alisema.

Alitaja sababu za kuchelewa zimetokana na kutowasilishwa na kuidhinishwa kwa usanifu wa mwisho wa mradi, janga la mafuriko Mto Rufiji pamoja na UVIKO-19.

Pia alisema kukatika katika kwa umeme kwenye mradi kumesababisha madai ya Dola za Marekani milioni 8.53 sawa na Sh. bilioni 19.51.

"Kukatika mara kwa mara kwa umeme eneo la Mradi wa Julius Nyerere kuanzia Januari 2020 hadi Oktoba 2020, kumesababisha mkandarasi kudai Dola za Marekani milioni 8.53. hii ilisababishwa na kukosa tathmini iliyoainisha mahitaji ya umeme kuendeshea vifaa vya mkandarasi kwenye eneo la mradi," alisema na kubainisha kuwa hatua hiyo ilisababisha kuongezeka gharama na muda wa kukamilisha mradi.

**MIRADI ILIYOTELEKEZWA**

CAG Kichere pia alisema kuna miradi ya barabara iliyotelekezwa yenye thamani ya Sh. bilioni 3.09.

"Makandarasi wanne walitelekeza miradi ya ujenzi wa barabara yenye thamani ya Sh. bilioni 3.09 uliokabidhiwa na TARURA (Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini) kabla ya miradi hiyo kukamilika kwa mujibu wa mikataba," alisema.

Mwaka 2019/20, alisema TARURA ilitelekeza miradi ya barabara yenye thamani ya Sh. bilioni 1.95 na kwamba inaonyesha tatizo halijapatiwa ufumbuzi.

**LIGANGA NA MCHUCHUMA**

Alisema pia amebaini upungufu unaochelewesha utekelezaji wa mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga ikiwamo serikali kuchelewa kufanya uamuzi.

"Pia haikutoa tangazo linalohalalisha utoaji wa vivutio vya uwekezaji vilivyoainishwa kwenye mkataba wa utendaji kazi, hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mradi, pia kutolipwa kwa fidia ya ardhi kwa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 13.52, gharama ya kulipa fidia ya Sh. bilioni 4.8 kwa Mchuchuma na Sh. bilioni 8.84 Liganga hazikulipwa kwa wananchi wanaoishi jirani na eneo la mradi, kwa miaka sita, ucheleweshaji huu unaathiri utekelezaji wa mradi," alisema.

**VICHWA TRENI NA MABEHEWA**

Alisema kuchelewa kuwasili kwa vichwa vya treni viwili na mabehewa 12 ya abiria, mkataba wa Shirika la Reli Tanzania na kampuni ya Uturuki ilitaka vichwa na mabehewa kwa ajili ya majaribio ya treni ya kisasa ya mwendokasi kufika nchini Februari 28, mwaka 2021.

"Mzabuni aliongezewa muda hadi Desemba 31, mwaka 2021 hata hivyo hadi nakamilisha ukaguzi Februari 2022 vichwa vya treni na mabehewa havikuwa vimefika nchini," alisema.

Alisema kuchelewa kukamilika kwa mradi kumesababisha gharama za nyongeza Sh. bilioni 9.2.

Alibaini nyongeza ya muda ya miezi 35 kukamilisha sehemu ya kwanza ya ujenzi wa SGR hadi Septemba 23, mwaka 2022.

"Nyongeza ya muda ilitokana na upungufu kwenye usanifu wa mradi, kuchelewa kutatua changamoto ya njia kipande cha reli kuelekea bandarini na kusababisha ongezeko la gharama za mradi wa Sh.Bilioni 9.2 ambazo ni hasara kwa serikali," alisema.

**MIKOPO YA ASILIMIA 10**

CAG alisema ukaguzi umebaini mikopo ya Sh. bilioni 47.01 iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na Mamlaka 155 za Serikali za Mitaa haijarejeshwa.

Alisema Mamlaka za Serikali za Mitaa 83, hazikuchangia Sh. bilioni 6.68 ya asilimia 10 ya mapato yao ya ndani kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

# Rais ataka wananchi waelezwe chanzo kupanda bei ya bidhaa

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza watendaji wake kuwaeleza ukweli wananchi kinachoendelea duniani kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta kunakosababisha bidhaa nazo kupanda na kuacha kusubiri mpaka yeye azungumze.

Mkuu wa Nchi alitoa maagizo hayo jana mkoani Dodoma alipopokea ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka 2020/21.

"Tuseme yaliyoko duniani wananchi wajue mwenendo wa bei za dunia. Kwa mfano, ukiangalia Afrika Mashariki na Kati, Tanzania ndiyo yenye bei ya chini ya mafuta lakini wenye sekta hawasemi, wamejifungia tu, ikipanda wanapandisha tu.

"Semeni kwa wananchi nini kinatokea na kwa nini bei zinapanda, mpaka kila kitu Rais aseme, kila kitu ni Rais, huko mitandaoni Rais hajasema, Rais ni nani? Rais ni taasisi, ninyi ni wasaidizi wangu, saidieni kusema huko kila mtu kwenye sekta yake linapotokea awe mwepesi wa kusema tutaangaliana kwenye hilo," alionya.

Rais Samia alisema kwa sasa maoni mengi ya Watanzania kwenye mitandao ya kijamii yanahusu kupanda kwa bei ya bidhaa.

"Wote tunajua kwamba baada ya UVIKO-19, dunia yote imekuwa na mfumuko wa bei kwa sababu bidhaa zote zilizokuwa maghalani zilitumika ndani ya miaka hii miwili, mitatu ambayo dunia imekumbwa na janga hili na hakukuwa na uzalishaji.

"Uzalishaji ndiyo unaanza sasa, kwa maana hiyo kama bidhaa ni chache duniani bila shaka bei zitapanda, zimepanda kwa bidhaa nyingi tunazoagiza kutoka nje, lakini lipo suala la upandaji wa bei za mafuta," alifafanua.

Rais Samia alisema mafuta yamekuwa yakipanda tangu katikati ya mwaka jana na serikali kwa mara ya kwanza ilichukua hatua ya kupunguza tozo ili kushusha gharama kwa wananchi ingawa yameendelea kupanda.

"Waziri alichukua hatua kipindi hiki cha pili lakini yamepanda kwa Sh. 156 kwa lita, waziri akaona nikitoa Sh. 100 yapande kwa Sh. 56 nitaleta unafuu ndani ya nchi, lakini kwa bahati mbaya hakuangalia kwa upana zaidi kwamba ile ilikuwa tayari kwenye bajeti iliyopitishwa na Bunge.

"Kwa hiyo kulikuwa na utata kidogo, tumekaa kama serikali tumerekebisha ile shilingi iliyotoka nimeagiza irudishwe, tathmini tuliyofanya hata kama ile shilingi tungeitoa kwa mwenendo wa upandaji wa mafuta duniani bado isingekuwa na matokeo ila tungejikosesha tunachokusanya," alisema.

Rais alisema wameamua shilingi iliyotolewa irudishwe lakini wabunge kwenye maeneo yao na mawaziri wanaosimamia sekta wawaeleze wananchi ukweli kuwa vita vya Russia na Ukraine vimepandisha bei ya mafuta.

"Mafuta yanapopanda ndiyo kila kitu kinapanda, nauli zitapanda, usafirishaji bidhaa utapanda, sasa hivi kutoa kontena la bidhaa kutoka China kulileta Tanzania wafanyabiashara walikuwa wanalipa Dola za Marekani 1,500 kwa kontena la futi 40 lakini kwa sasa ni Dola 8,000 hadi 9,000.

"Hii inakwenda kuingia kwenye bidhaa zinazoletwa, kwa hiyo waambieni wananchi ukweli wasikae kulaumu serikali haisemi kitu, bei zinapanda za mafuta, mafuta ya kula yamepanda," aliagiza.

Kuhusu mafuta ya kula, Rais Samia alisema kuwa alimwagiza Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, katika bajeti ya fedha inayoishia ya mwaka 2021/2022 na ile ya mwaka ujao wa fedha, waingize kitu ili kulinda viwanda vya ndani kwenye uzalishaji.

Alisema pamoja na kuongeza hicho kitu na kuzuia mafuta ya nje yasije nchini, viwanda vya ndani vimefungwa hakuna uzalishaji.

"Ninaomba litazameni tena kama haitusaidii, ondoeni ili mafuta ya nje yaingie angalau hata bei ikiwa kubwa lakini wananchi wana mafuta ya kutumia.

"Mmezuia mafuta ya nje hayaingii, ndani hayazalishwi wananchi wanapiga kelele bila shaka mafuta yatapanda kwa kiasi kikubwa," alisema.



CAG Kichere (kulia), akiwa na viongozi mbalimbali waliohudhuria kabla ya kuwasilisha Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2020/2021, Ikulu ya Chamwino, jana. **PICHA: IKULU**

# Miradi 222 yenye viashiria vya ubadhirifu kuchunguzwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imebaini miradi ya maendeleo 222 yenye thamani ya Sh. bilioni 79.14 ina viashiria vya ufujaji na ubadhirifu wa fedha, hivyo kuanza uchunguzi.

Akiwasilisha ripoti ya taasisi hiyo kwa Rais Samia Suluhu Hassan Ikulu Chamwino jana, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna wa Polisi, Salum Rashid Hamduni, alisema kwa kipindi cha mwaka 2020/21, taasisi hiyo imefuatilia miradi ya maendeleo 1,188 katika sekta za ujenzi, maji, elimu, afya na kilimo yenye thamani ya Sh. bilioni 714.17 kwa mujibu ya mikataba.

Alisema katika ufuatiliaji huo miradi 969 yenye thamani ya Sh. bilioni 635.09 ilibainika kuwa na mapungufu madogo na kuwashauri watekelezaji wake namna bora ya kutekeleza miradi hiyo.

"Kati ya miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji ipo 222 yenye thamani ya Sh. bilioni 79.14 ilionekana kuwa na viashiria vya ufujaji na ubadhirifu wa fedha na katika eneo hili uchunguzi ulianzishwa na unaendelea,"alisema.

Katika uchambuzi wa mifumo, Mkurugenzi huyo alisema kazi 683 zilifanyika kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kushauri namna bora ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika.

"Tulifanya uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji wa ushuru wa huduma katika halmashauri 141 nchini, tulifanya uchambuzi wa mfumo wa utoaji na urejeshaji mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, uchambuzi wa mfumo wa utoaji wa vibali vya ujenzi katika halmashauri 102,"alisema.

Kuhusu uchunguzi na huduma za sheria, Mkurugenzi huyo alisema Sh. bilioni 29.3 zimeokolewa na taasisi hiyo na kufanya uchunguzi na kukamilisha majalada 1,053 ya makosa ya rushwa ikiwamo majalada tisa ya rushwa kubwa.

"Rushwa kubwa ni zile chunguzi za tuhuma za rushwa zenye thamani ya Sh. bilioni moja au zaidi, pia tumekamilisha majalada 28 yaliyotokana na taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), pia kesi 503 ziliamualiwa mahakamani ambapo Jamhuri ilishinda 347 sawa na asilimia 68.9 na kushindwa kesi 156 sawa asilimia 31.1," alisema.

Hata hivyo, alisema kesi 544 zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini zikiwamo kubwa nne.

"Takukuru kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeweza kutaifisha mali mbalimbali zenye jumla ya Sh. bilioni 1.2, pia iliweka zuio la fedha Sh. milioni 495.5 pamoja na mali zenye thamani ya Sh. bilioni 2.6 ikiwamo nyumba 15 zipo maeneo mbalimbali nchini, magari matatu,"alisema.

Hata hivyo, alisema taasisi hiyo iliwasiliana na Waajiri wa watumishi wa umma 257 ambao wana kesi mahakamani ili hatua za nidhamu zichukuliwe kwa mujibu sheria na taratibu za utumishi wa umma.


**BANI INVESTMENT LIMITED**

**DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS**

**NOTISI YA SIKU 14 / TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA NMB MAKAO MAKUU** tunatoa notisi ya siku 14 na tangazo la mnada wa hadhara wa mali zilizoorodheshwa hapo chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo. Hivyo basi utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada.Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| JINA LA MDAIWA | AINA YA MALI INAYOUZWA | MAHALI ILIPO | TAREHE |
|---|---|---|---|
| Berkeley Electrical Limited | Nyumba iliyoko kwenye kiwanja na.245 CT N o. 186153/15 .L.O No.26359,Sqm 1814.34 ($M^2$) | Msasani Regent Estate area,mtaa wa Vikawe -Dar es Salaam | 23.4.2022 |
| Juliana Input Co./Atupakisye Josiah Mwamgogwa | Nyumba yenye C.T No. 17617 - MBYLR, kiwanja No. 123, kitalu na. "LL" | Iwambi -Mbeya | 30.4.2022 |
| Seleman Said A lly | Nyumba | Busokelo-Tukuyu Mbeya | 14.5.2022 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Nyumba zitauzwa "kama zilivyo " as where is basis"
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyumba/kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:**

BANI INVESTMENT LTD, S.L.P 71340 Dar es Salaam Lida Building, ghorofa ya 3 chumba No. 0313 Nkrumah Street. Tel. 0713 224 578, 0754 688059, 0713 295747

# Ummy akiri huduma mbovu za afya hospitali za serikali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amekiri kuwa huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya vya serikali ni mbovu licha ya kuwekeza fedha nyingi katika kuboresha miundombinu, vifaa tiba na dawa.

Pia amesema serikali inafanya mapitio ya gharama za matibabu katika hospitali na vituo vya afya vya umma kwa watu wanaolipa fedha taslimu ili kuondoa vikwazo vya gharama kubwa za matibabu.

Ummy alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akifungua mkutano wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Wizara ya Afya.

Alisema pamoja na serikali kuwekeza fedha nyingi katika sekta ya afya, bado utoaji wa huduma katika hospitali na vituo vya afya ni mbovu.

"Wakati tunajisifia kuwa tumepata mafanikio, Watanzania wamekuwa wanatushangaa pamoja na kutumia fedha nyingi katika kuwekeza katika sekta hii, huduma bado ni mbovu.

"Hivi sasa serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya dawa lakini bado kuna malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu kupata dawa katika hospitali na vituo vya afya vya serikali. Watu hawapati dawa, lakini suala la huduma kwa wateja bado ni kero kulinganisha na hospitali za binafsi," alisema Ummy.

Sambamba na hilo, Ummy aliwataka watumishi wa afya wa serikali kuacha kufanya kazi kwa mazoea na kila mmoja amsimamie mwenzake na atakayekwenda kinyume awajibishwe.

"Kwa nini daktari huyo huyo akiwa katika hospitali binafsi anakuwa na kauli nzuri kwa wateja, lakini akiwa katika hospitali za serikali anakuwa na kauli mbovu kwa wateja? Mgonjwa anakwenda hospitali binafsi anahudumiwa vizuri lakini huku kwetu huduma ni mbovu," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliwaagiza watumishi wa afya kuwa wabunifu katika kuweka utaratibu mzuri wa kutoa huduma kwa wateja ili kuongeza mapato.

"Watu wengi hivi sasa wanakwenda katika hospitali za binafsi kutokana na kupatiwa huduma nzuri. Lakini kama mtaweka mazingira mazuri, lazima wataanza huku badala ya kwenda katika sekta binafsi na ninyi kupata mapato ambayo yatawasaidia kuhudumia wale watu wa msamaha," alisema.

Pia aliagiza kuandaliwa kwa utaratibu wa kila kituo cha afya au hospitali ya serikali kuwapo na duka la dawa ili kuondoa kero iliyoko hivi sasa ya wagonjwa kukosa dawa.

Akizungumzia kuhusu kufanya mapitio ya gharama za matibabu kwa hospitali na vituo vya afya vya serikali, alisema ndani ya miezi mitatu wanatarajia kutoa mwongozo utakaoelekeza kiasi cha malipo kwa huduma mbalimbali.

"Mwongozo uliopo ni wa muda mrefu na umepitwa na wakati. Sasa tunakwenda kufanya mapitio ya gharama kama mtu anataka kumwona daktari ni kiasi gani anapaswa kulipa kwa zahanati, kituo cha afya, hospitali za rufani za mikoa au zile za kanda ili kuondoa kero iliyopo hivi sasa ya watu kijipangia kiholela kiasi kikubwa cha fedha," alibainisha.

Pia alisema katika uongozi wake kwenye wizara hiyo, vipaumbele vyake ni huduma bora za afya, bima ya afya kwa wote na huduma za kinga.

"Nataka katika awamu hii ambayo nimerudi Wizara ya Afya, tupimwe katika mambo haya. Ni lazima huu mchakato wa kila Mtanzania kuwa na bina ya afya, ukamilike kwa muda mfupi ili kuondoa changamoto za matibabu kwa fedha mkononi," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alisema baraza hilo litajadili mpango na makadirio ya bajeti ya mwaka 2022/23 na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/22.

Alisema lengo la wizara hiyo ni kutoa huduma bora za afya, kinga, vipimo, upasuaji, huduma za kansa na kukomesha malalamiko ya kukosa dawa kwa wagonjwa katika hospitali na vituo vya afya vya serikali.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa OPEC Fund, Dk. Abdulhamid Al Khalifa (wa pili kushoto), alipofika Ikulu Zanzibar jana kwa mazungumzo akiwa na ujumbe wake. **PICHA: IKULU**

# Basi lililosababisha ajali Morogoro lilitengenezwa kwa vifaa vya ujenzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UCHUNGUZI uliofanywa na Jeshi la Polisi kuhusu basi lililosababisha ajali na kuua watu kadhaa mkoani Morogoro, limedaiwa kuwa lilitengenezwa kwa kutumia vifaa vya ujenzi.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, alisema hayo jana mbele ya waandishi wa habari wakati akitoa taarifa ya utafiti wa vyanzo vya ajali uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema kwa mujibu wa uchunguzi huo, baadhi ya vifaa vilivyofungwa kama 'ringboard', hutumika katika kuweka zege kwenye ujenzi wa nyumba.

"Hizi ni 'ringboard' ambazo hutumika kuweka zege katika nyumba ndizo zimewekwa kwenye 'chesis' ya gari na hizi ndizo zimekata viungo vya Watanzania," alisema Masauni.

Kutokana na kubainika kasoro hiyo, aliagiza mmiliki wa gari na kiwanda kilichofunga kifaa hicho, wakamatwe mara moja na washtakiwe huku akiagiza msako ufanyike nchi nzima kwa gari lolote lililofanya mambo kama hayo pia lichukuliwe hatua.

Pia aliagiza kuanzia sasa Jeshi la Polisi lianze operesheni maalum ya usalama barabarani itakayohusisha doria na mambo mengine ili kurudisha hali ya nidhamu barabarani. Alisema operesheni hiyo itaongeza kasi katika ufanisi wa kusimamia sheria.

Sambamba na hilo, alisema umefika wakati kwa Jeshi la Polisi kupitia upya utaratibu mzima wa utoaji mafunzo ya udereva kwa kukagua vyuo vyote vinavyotoa mafunzo hayo kama vinakidhi mahitaji yaliyopo.

"Tunataka kuwa na madereva wanaoingia barabarani wakiwa wanatambua thamani ya kazi yao. Hata wale waliosababisha ajali lazima wafanyiwe uchunguzi kujua leseni zao wamezipata wapi na chuo gani wamesoma," alisisitiza.

**VYANZO VYA AJALI**

Kuhusu vyanzo vya ajali, Masauni alisema utafiti wa UDSM umebaini kuwa unatokana na mambo makuu matatu ambayo ni uzembe wa madereva, uchakavu wa magari na miundombinu ya barabara.

Alisema kupitia utafiti huo, uzembe wa madereva unachangia ajali kwa asilimia 76 huku ubovu wa mabasi asilimia 18 na miundombinu asilimia 16.

"Unakuta dereva anaendesha gari kinyume cha kiwango cha mwendo ambao umewekwa, mwingine kalewa au anataka kuyapita magari bila sababu za msingi. Hiyo ni kinyume cha sheria," alisema Masauni.

Kutokana na hilo, Waziri Masauni aliagiza Jeshi la Polisi kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani kuanzia leo, mabasi yote na maroli yawe na vidhibiti mwendo kwa sababu baadhi ya wamiliki wa vyombo vya usafiri wanapoingiza vyombo hivyo, wamekuwa wakitoa vidhibiti mwendo.

Alisema hiyo tafsiri yake wana dhamira mbaya ya kukiuka sheria kwa sababu vidhibiti mwendo vimewekwa kwa ajili ya kulinda usalama barabarani.

# Prof. Ngowi, dereva wake kuagwa leo Dar es Salaam

**Na Waandishi Wetu**

MIILI ya wafanyakazi wawili wa Chuo Kikuu Mzumbe; Mkuu wa Ndaki ya Dar es Salaam, Prof. Honest Ngowi na dereva wake Innocent Mringo, inatarajiwa kuagwa leo kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam kabla ya kusafirishwa kwenda Moshi mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya maziko.

Wawili hao walifariki dunia Jumatatu kwa ajali ya gari iliyotokea Mlandizi mkoani Pwani walipokuwa safarini kwenda mkoani Morogoro.

Akizungumza kwa niaba ya Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Mzumbe jana, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa chuo hicho, Rose Joseph, alisema hafla ya kuaga miili hiyo imelenga kutoa heshima za mwisho kwa marehemu hao kama watumishi wa umma na vilevile kama wanataaluma.

Alibainisha kuwa baada ya kuaga miili hiyo, mwili wa Mringo utasafirishwa siku hiyo hiyo kwenda nyumbani kwao Marangu Mwika, Moshi kwa ajili ya maziko yanayotarajiwa kufanyika kesho huku mwili wa Prof. Ngowi ukitarajiwa kufanyiwa ibada ya kifamilia kesho na baadaye jioni kusafirishwa kwenda mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya maziko yatakayofanyika Jumamosi kijijini kwao Singa Kati, Kibosho.

"Kama taasisi tumeamua kuwapa heshima ya kuwajumuisha pamoja kwa sababu wamepata ajali pamoja na kufariki dunia pamoja, ili baadaye tuzipe familia nafasi ya kuwaaga kipekee na baadaye wapumzishwe kwa amani," alisema Rose.

Aliwashukuru watu wote waliofanya kazi kwa karibu na Prof. Ngowi na Mringo na kazi walizofanya wataendelea kuzienzi wakati wote na hazitakuwa bure.

Prof. Ngowi aliyekuwa mbobevu wa masuala ya uchumi na biashara, mbali na kutoa elimu hiyo darasani, alikuwa akielimisha jamii kupitia majukwaa mbalimbali na kwenye vyombo vya habari.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na chuo hicho kwa ajili ya kuaga miili ya wawili hao, shughuli ya kuaga itaanza majira ya 3:00 asubuhi hadi saa 8:20 alasiri.

●**Imeandikwa na Idda Mushi (MOROGORO) na Jenifa Gilla (DAR)**

HABARI KITAIFA

# Mifumo ya ardhi kuwa ya kidigitali

**Na Munir Shemweta,** DODOMA



WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Korea Kusini, imeanzisha mkakati wa kubadili mifumo yake ya upangaji, utumiaji, upimaji na uwekaji kumbukumbu kutoka analogia kwenda digitali.

Hatua hiyo inatokana na wizara kuendelea kutumia mifumo ya analogia katika upangaji, utumiaji, upimaji na uwekaji kumbukumbu za sekta ya ardhi.

Katika kufanikisha azma hiyo, Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Korea Kusini, zimeingia makubaliano ya ushirikiano wa utekelezaji mradi wa ujenzi wa kituo cha kisasa cha mafunzo na uboreshaji miundombinu ya ardhi.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi (pichani), alisema hayo jana wakati akielezea ushirikiano baina ya Korea Kusini na wizara katika uanzishaji kituo cha mafunzo kwa wataalamu wa upimaji na uboreshaji miundombinu ya sekta hiyo.

Uanzishwaji kituo cha kisasa utagharimu Sh. bilioni 5.2 na ule wa ujenzi wa miundombinu utagharimu dola milioni 64.

Dk. Kijazi alisema uanzishwaji wa kituo hicho si tu kwa ajili ya kutumia teknolojia ya kisasa pekee bali itakayoendana na wakati na kupitia mradi huo, wizara itapokea msaada wa kiufundi na wataalamu wake kupatiwa mafunzo na kuwekewa vifaa vinavyohusu mifumo ya ardhi.

"Pamoja na kuwekwa vifaa kwenye kituo pia watumishi watajengewa uwezo na kukusanya, kuchakata na kutumia takwimu za ardhi katika mipango ya kuendeleza sekta ya ardhi," alisema.

Dk. Kijazi alisema sehemu ya pili ya mradi huo itakuwa ujenzi wa miundombinu itakayowezesha wizara kutumia teknolojia ya kisasa katika kupanga, kupima na kutumia takwimu za ardhi kwenye maeneo mbalimbali ya nchi.

Mradi mzima utahusisha uandaaji ramani za uwiano mdogo na zile za uwiano mkubwa kwa miji mikuu ya mikoa 26 ya Tanzania Bara sambamba na kuweka vituo vya kielektroniki vya upimaji ardhi na kuboresha miundombinu ya kusambaza taarifa za kijiografia kwa idara za serikali na watumiaji wote nchini.

Katika hatua nyingine, ujumbe wa wataalamu kutoka Korea Kusini uliokuja kwa ajili ya hatua za awali za utekelezaji miradi hiyo, ukiongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hojung Solution Co. Ltd, Munseok Lee, umekutana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, kwa ajili ya kujitambulisha na kumwelezea maendeleo ya utekelezaji miradi hiyo.

Ujumbe huo ulimweleza Dk. Mabula kuwa uko tayari kuanza utekelezaji wa mradi huo baada ya maandalizi ya awali ya kutoa mafunzo kwa baadhi ya watumishi nchini.

Dk. Mabula aliuambia ujumbe huo kuwa ana imani ulishiriki vyema hatua zake za awali za maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo na kwamba matarajio yake kila kitu kitakwenda vizuri katika utekelezaji mradi huo.

# Sera elimu yataka umri wa elimu lazima kuwa miaka 10

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeunda timu ya kuanza kupitia Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 ambayo miongoni mwa mambo yanayotajwa kwenye sera hiyo ni elimu ya lazima kuwa miaka 10 badala ya saba.

Hatua hiyo itakwenda sambamba na mabadiliko ya mitaala ya elimu kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya walimu.

Waziri wa Wizara hiyo, Prof. Adolf Mkenda (pichani), aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa kupokea maoni kuhusu uboreshaji wa mitaala na sera ya elimu kutoka kwa viongozi wa dini na wamiliki wa shule binafsi, jijini hapa.

Alisema pamoja na kuendelea na mchakato wa kuboresha mitaala, ameona ni vyema kufanya mapitio ya sera ili kwenda sambamba na maboresho hayo na tayari ameshaunda timu ambayo imepewa jukumu la kupitia sera ambayo ni tofauti na ile inayosimamia maboresho ya mitaala.

Pia alisema sera hiyo imebainisha kuwa mtoto wa kitanzania mwenye miaka kati ya minne hadi sita, angalau asome elimu ya awali kwa pamoja na elimu ya msingi kwa miaka 10 ili kumwezesha kujua kusoma, kuandika na kupata ufahamu wa mambo yatakayompa maarifa.

"Baadhi ya maeneo hayajatekelezwa kwenye hii sera, hivyo nimeona tufanye mapitio na kama tuendelee kuutekeleza au kama tubadilishe basi tubadilishe nini. Tunapotekeleza elimu ya lazima basi tutatekelezaje bila kushusha kiwango. Tumeunda timu ya sera itakayoongezwa na profesa wa uchumi pamoja na mambo mengine waje na mapendekezo.

"Kama tunaenda nayo, tunaandika sera upya au tunaboresha katika maeneo yanayofaa au tuondoke kabisa. Pia wataangalia tunahitaji walimu wangapi, fedha kiasi gani, wataalamu wangapi na madarasa mangapi. Hatua hii inalenga kuwaandaa wanafunzi wa kitanzania katika kuakisi mazingira ya Tanzania na kimataifa," alisema.

Awali, Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa wa Watanzania kutoa maoni ya kuboresha mitaala na mpaka sasa zaidi ya wadau 100,000 wameshajitokeza kutoa maoni yao.

Alisema katika maeneo ambayo Watanzania wameyatolea maoni ni pamoja na kupendekeza kuondolewa kwa wingi wa maudhui, kufundisha masomo ya ujuzi kulingana na mazingira, kuwapo na mikondo ya kubaini vipaji vya wanafunzi, lugha zote zitumike na kusisitiza kufundisha maadili kuanzia ngazi ya awali.

Dk. Mtahabwa alisema lengo la wizara ni kuhakikisha Januari, 2024 mtaala mpya uanze kutumika kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya walimu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Anneth Komba, alisema mapitio ya mitaala imepita hatua mbalimbali za maboresho na kuwa matarajio ni kuwa rasimu ya kwanza ya mtaala itakuwa tayari ifikapo Mei 30, mwaka huu na wadau wanataka fursa ya kupitia na kuboresha zaidi.


## TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA

### TAARIFA YA UPANUZI WA MASHIMO YA GENA NA GOKONA YALIYO KATIKA MGODI WA DHAHABU WA NORTH MARA, WILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA

Mradi pendekezwa wa upanuzi wa mashimo ya Gena na Gokona (Mradi) upo ndani ya Wilaya ya Tarime katika Mkoa wa Mara nchini Tanzania. Mradi pendekezwa unamilikiwa na Mgodi wa Dhahabu wa North Mara (NMGM) ambayo ni kampuni ya utafutaji na uchimbaji madini inayomilikiwa na kampuni ya Twiga Corporation, iliyoundwa kwa ubia kati ya Barrick (84%) na Serikali ya Tanzania kwa (16%). Eneo la Mradi liko chini ya Leseni ya Uchimbaji Maalum (SML 17/96). Mradi pendekezwa unazigusa kata nne ambazo ni Nyamwaga, Nyarokoba, Kibasuka na Kemambo pamoja na sehemu za vijiji vitano: Komarera, Genkuru, Msege, Kewanja na Nyakunguru.

Upanuzi wa mashimo ya Gena na Gokona ni muendelezo wa shughuli za uchimbaji pamoja na faida za kiuchumi zitokanazo na shughuli hizo za uchimbaji. Kwa miaka mingi, NMGM imekua ikiendeleza tafiti katika eneo hilo ambazo zimeonyesha uwepo wa mashapo yaliyopo kwenye mashimo hayo.

Ili kutekeleza Mradi pendekezwa, Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) itafanyika kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Kanuni za Tathmini ya Athari za Mazingira ya mwaka 2005 na marekebisho yake ya mwaka 2018 pamoja na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

NMGM imeziteua kampuni za Digby Wells Environmental na PAULSAM Geo-Engineering Limited kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Utafiti huo utachunguza athari chanya na hasi kwenye mazingira na jamii zitakazotumika kuunda Mpango wa Usimamizi wa Mazingira kwenye utekelezaji wa Mradi.

Kwa kuzingatia utaratibu, usajili pamoja na uwasilishwaji wa taarifa za awali za mradi kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) unaendelea kama sehemu ya TAM. Tangazo hili linawakaribisha watu wote wenye nia, ushauri au maarifa kuhusu athari zozote ama za kimazingira au kijamii zinazohusiana na mradi huu kuwasilisha mawazo yao kwa kupitia anuani zifuatazo:

| Mdhibiti | Muwekezaji | Wataalamu washauri elekezi |
|---|---|---|
| Mkurugenzi Mkuu<br>Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC),<br>S.L.P. 63154, Regent Estate,<br>Dar es Salaam, Tanzania.<br>Simu: +255 22 2774889<br>Barua pepe: dg@nemc.or.tz | Mgodi wa Dhahabu wa North Mara (NMGM)S.L.P. 422<br>Tarime<br>Tanzania<br>Faksi: 255282621903<br>barua pepe: apolinary.lyambiko@barrick.com | PAULSAM Geo-Engineering Company Limited,<br>Ghorofa ya 07 , Faykat Tower Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam, Tanzania.<br>S.L.P. 70812<br>Simu/Faksi: +255 755561188<br>Barua pepe: piliseleman@gmail.com<br><br>ESD Advisory Ltd T/A Digby Environmental<br>Madai Crescent, Plot 151, Ada Estate, Dar es Salaam.<br>Jamii:+255717087482<br>Barua pepe: Deogratius.lorri@digbywells.com |

**Ushirikishwaji wa wadau utafanyika kama sehemu ya mchakato wa TAM ambapo habari zaidi zinazohusiana na mradi zitawasilishwa.**

216778302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Karibu sana DRC EAC

**JUMUIYA** ya Afrika Mashariki imepata nguvu mpya, baada ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kujiunga rasmi kama mwanachama mpya, hivyo kuifanya iwe na wanachama saba.

Jumuiya hii inahistoria ndefu ya kuvuka milima na mabonde kabla na baada ya kuanzishwa mwaka 1967, kuvunjika mwaka 1977 na kufufuliwa tena mwaka 1996. Safu hii haitoshelezi kueleza njia iliyopitia hadi sasa, lakini itoshe tu kwa kusema kwamba inazidi kuimarika na kupanuka.

Ilipoanzishwa ilikuwa inaundwa na mataifa matatu ya Tanzania, Kenya na Uganda huku Burundi na Rwanda zikiongezeka mwaka 2007, na baadaye Sudan Kusini kujiunga mwaka 2016. Kuongezeka kwa nchi hiyo katika jumuiya pia kutaongeza idadi ya watu, kwa kuzingatia kuwa DRC ni moja ya mataifa ya Bara la Afrika yenye idadi kubwa ya watu.

Kwa sasa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinakadiriwa kuwa na raia wapatao milioni 193 na kujiunga kwa DRC kutaongeza idadi hiyo na kufikia watu milioni 280, hivyo na kufanya mwingiliano wa kibiashara kuwa mkubwa zaidi.

Kadhalika, hatua hii ni fursa muhimu katika kukuza uchumi na maendeleo ya eneo hilo kwa kutilia maanani kwamba nchi wanachama zitatumia pamoja rasilimali zinazopatikana kila nchi, zikiwamo zinazopatikana katika DRC kama madini ya aina tofauti, mazao ya misitu (mbao) na ardhi yenye rutuba na mafuta.

Haya ni mambo yanayodhihirisha kwamba EAC itaweza kusonga mbele kwa kuunganisha nguvu miongoni mwa nchi wanachama, hivyo kutimiza malengo ya jumuiya ya kuziendeleza kiuchumi na kuwaletea maendeleo watu wake.

Watu kadhaa waliotoa maoni yao baada ya DRC kuridhiwa rasmi kuwa mwanachama mpya wa jumuiya hiyo, walieleza kuwa hiyo ni fursa kubwa kwa taifa hilo na EAC kwa ujumla kwamba; hatua hiyo itapanua wigo wa biashara, kuanzia vikwazo mipakani pamoja na utekelezaji wa miradi kwa pamoja husan ya miundombinu kama barabara na reli.

Ikumbukwe kwamba DRC licha ya kuwa na utajiri mkubwa wa rasilimali, inakabiliwa pia na kutokuwa na miundombinu ya usafiri na usafirishaji kama barabara na reli tangu kupata Uhuru mwaka 1960, hivyo kupitia miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa nchi za EAC, itanufaika kwa fursa hiyo.

Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Peter Mathuki, akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha baada ya wakuu wa jumuiya hiyo kupitisha nchi hiyo ijiunge rasmi, alisema tukio hilo ni kubwa na heshima kwa jumuiya kulialika rasmi taifa hilo kuwa mwanachama wake mpya.

Alisema ni furaha yao na wananchi kupitia kujiunga kwa taifa hilo kutaongeza fursa za kiuchumi na kibiashara katika kusafirisha bidhaa kuanzia Bahari ya Hindi hadi Bahari ya Atlantic.

Alisema nchi hizo zikikubaliana kuondoa vikwazo mipakani katika biashara zitaongeza nafasi kwa wananchi wa Jumuiya hiyo.

Hata hivyo, kikwazo kikubwa kinachoendelea kuwa tishio kwa nchi hiyo ni kukosekana kwa usalama wa watu husan maeneo ya magharibi, ambapo makundi yenye silaha yamekuwa yakijihusisha na vitendo vya mauaji ya raia. Hivyo kuufanya Umoja wa Mataifa (UN) kutuma vikosi vya ulinzi wa amani, ingawa hatua hiyo haijamaliza tatizo.


Tunaamini kuwa suala la usalama wa DRC linajulikana, hivyo EAC italipatia kipaumbele ili taifa hilo lipate amani ya kudumu na kushiriki ipsavyo katika shughuli zote kwenye mtangamano huo.

Tunakuwa na matumaini ya nchi hiyo kusaidiwa na kuhakikishiwa usalama wake ndani ya EAC kufuatia kauli ya Dk. Mathuki kusema kuwa kuhusu masuala ya kiusalama, nchi hizo zitafanya jitihada za pamoja kuunganisha nguvu kuhakikisha wanadumisha usalama na amani katika nchi hiyo.

Kwamba kwa pamoja zitajitahidi kuwasaidia kuona DRC inaondokana na changamoto za kiusalama zilizoko katika nchi hiyo kwa umoja kama nchi za EAC.

Tunaikaribisha sana DRC ndani ya jumuiya tukiamini kuwa kuna mambo mengi nchi wanachama zitanufaika nayo na vilevile nayo itanufaika sana kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Jicho kulinda uchumi lielekezwe ajali barabarani, ripoti inatisha

Na Christina Mwakangale

**UNAPOZUNGUMZIA** uchumi wa taifa upo mchango mkubwa utokanao na sekta ya usafirishaji na uchukuzi, iwe kwa kutumia barabara, maji au anga.

Nchi za Afrika au zinazoendelea shughuli za usafiri wa abiria hata uchukuzi tegemeo ni barabara, hivyo matumizi yake hayaepukiki, iwe watu binafsi au taasisi.

Usafirishaji mizigo pia kwa nchi hizo ikiwamo Tanzania kutoka ilipofika hasa inayofikia bandarini, uchukuzi wake ni wa malori ambayo hubeba makontena ya mizigo hiyo kuelekea maeneo tofauti ndani na nje ya nchi.

Safari nyingi za mizigo hiyo hufanyika mara nyingi usiku, serikali ikiona ni muhimu kupishana na shuguli za mchana kutwa zinazofanywa na magari madogo na hata watumiaji wengine wa barabara.

Wiki hii imetokea ajali ambayo imehusisha gari la mizigo lenye kontena pamoja na gari alilokuwa akitumia Mkuu wa Chuo cha Mzumbe Kampasi ya Dar es Salaam, Prof. Honest Ngowi, ambaye uhai wake umekatizwa na ajali hiyo pamoja na dereva wake.

Ajali hiyo ilitokea eneo la Miwaleni, wilayani Kibaha mkoani Pwani, kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Pius Lutumo.

Si ajali hiyo tu zipo nyingi ambazo hutokea maeneo tofauti, Mbeya pia wiki hii lori la mizigo limesababisha vifo vya watu watano baada ya ajali kutokea eneo la Iwambi, jijini Mbeya, kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Ulrich Matei.

**Si ajali hiyo tu zipo nyingi ambazo hutokea maeneo tofauti, Mbeya pia wiki hii lori la mizigo limesababisha vifo vya watu watano baada ya ajali kutokea eneo la Iwambi, jijini Mbeya, kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Ulrich Matei.**

Hizo ni ajali chache kati ya nyingi zinazotokea nchini kutokana na sababu tofauti, huku vyanzo pia vikiwa tofauti lakini kati ya hizo huchangiwa na magari hayo ya mizigo.

Ni jana tu iliwasilishwa ripoti ya utafiti uliofanywa na wasomi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambao waliweka wazi robo tatu ya ajali hutokana na uzembe katika uendeshaji na robo moja inayobaki ni kwenye ubovu wa magari na miundombinu duni.

Ukishuhudia palipotokea ajali iliyohusisha lori na gari ndogo madhara huwa zaidi kwa waliopo kwenye gari ndogo. Hatari za ajali za barabarani katika nchi zinazoendelea ziko kiwango cha juu kwa mara tatu zaidi.

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), inasema kwamba kuna vifo 27 kwa kila watu 1000.

Vifo vya barabarani katika nchi za Afrika ni mara tatu zaidi ya ajali zinazotokea Ulaya, ambako kuna ajali chache.

Ripoti inasema, karibu nusu ya mataifa 54 ya Afrika, hayana sheria za mwendo kasi katika nchi zao.Botswana, Ivory Coast na Cameroon, ni miongoni mwa nchi ambazo kiwango cha vifo kinaongezeka kutokana na ajali.

Kwa miezi sita ya mwanzo ya mwaka 2020, ripoti hiyo inaonyesha kwamba malori yaliyohusika katika ajali ni 167 na kusababisha vifo vya watu 130 na majeruhi 142, wakati daladala za abiria zilipata ajali 143, na kusababisha vifo 89 na majeruhi 268.

Ipo haja ya safari za kusafirisha mizigo hii ikawa na muda maalum, ili kuepusha hilo kwa kuwa utumiaji wa barabara hauepukiki na yapo maeneo ambayo barabara zake hutumika mara kwa mara.

Ajali za barabarani husababisha upotevu wa mali na rasilimali watu ambao ni tegemeo, ikitafsiriwa kuwapoteza athari huja kuanzia ngazi ya familia hadi taifa, kwa kuwa idadi ya wategemezi huongezeka ikiwamo gharama za matibabu.

# Nchi za EU zawekeza kampuni zaidi ya 100 nchini

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amesema nchi za Umoja wa Ulaya zimewekeza kampuni zaidi ya 100 nchini ambazo zimeajiri Watanzania kwa asilimia 98 na kati yao wanawake asilimia 38.

Alisema kampuni hizo zimewekeza katika sekta mbalimbali ikiwamo ya kilimo, utalii na madini.

Balozi Mulamula aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam, katika hafla ya uzinduzi wa ripoti kuhusu uwekezaji wa nchi za Umoja wa Ulaya nchini.

Alisema ripoti hiyo imeandaliwa tangu mwaka 2016 na imegusa sekta zote muhimu nchini.

"Ripoti hii imechukua muda mrefu kutokana na kuwapo kwa mabadiliko mbalimbali na maboresho ya uwekezaji katika mazingira ya uwekezaji nchini," alisema Balozi Mulamula.

Alisema historia inaonyesha Tanzania imekuwa na uhusiano mzuri na nchi za Ulaya, lakini kikwazo kilikuwa ni kuwa uhusiano wenye tija kwa taifa.

"Nimefarijika kupewa nafasi ya kumwakilisha Waziri Mkuu katika uzinduzi huu wa ripoti. Ujumbe kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kwamba tuwashike vizuri hawa wawekezaji kwa kuzingatia sera yetu inayoweka msisitizo katika diplomasia ya uchumi na nafarijika kama Waziri wa Mambo ya Nje," alisema.

Aliwataka Watanzania kutumia muda kusoma ripoti hiyo yenye takwimu za uwekezaji kwa Umoja wa Nchi za Ulaya waliowekeza nchini na namna ya kufikia fursa hizo.

Alisema serikali inaendelea kuwajengea uwezo Watanzania na kufikia kiwango cha mahitaji wanayotaka wawekezaji wakifungua masoko na kuwauzia bidhaa zao.

"Kutokana na ripoti hii iliyotuonyesha tulikotoka, tulipo na tunapoenda, hivyo sasa ni kuboresha mazingira ya kibiashara na kuongeza uwezo wa kuzalisha kwa wingi bidhaa zenye ubora," alisema Balozi Mulamula.

Alisema Tanzania imekuwa ikiuza bidhaa mbalimbali, lakini itauza bidhaa nyingi kulingana na makubaliano yaliyopo sasa.

"Kiukweli tupo pazuri na Rais alikutana na viongozi wa Ulaya kwa lengo la kuwahakikishia kuwa mazingira ni mazuri na nyumbani kumenoga hivyo njooni kuwekeza," alisema Balozi Mulamula.

Naye Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Manfredo Fanti, alisema ripoti ya biashara kati ya Tanzania na nchi hizo za Ulaya kwa mwaka jana, ilikuwa ni Euro milioni 856 kuja nchini na zilizoenda Ulaya kutoka Tanzania ni Euro milioni 456.

# Kortini wakikabiliwa mashtaka 746 kughushi, mmoja asomewa kitandani

**Na Kulwa Mzee**

SERIKALI imewafikisha mahakamani wafanyabiashara tisa wa Dar es Salaam wakikabiliwa na mashtaka 746 yakiwamo ya kughushi, kuwasilisha nyaraka za uongo na kutakatisha Sh. bilioni 4.78 mali ya Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Washtakiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ritha Tarimo na kusomewa mashtaka na Wakili wa Serikali, Faraji Nguka.

Wakili Nguka aliwataja washtakiwa kuwa ni Baraka Madafu, Mark Mposo, Lusekelo Mbwele, Leena Joseph, Benard Mndolwa, Salvina Karugaba, Mohammed Kombo na Hussein Amani.

Alidai mshtakiwa wa tisa, Paul Shayo yuko Hospitali ya Kitengule Tegeta na atasomewa mashtaka akiwa hospitalini.

Nguka akiwasomea washtakiwa wengine alidai shtaka la kwanza linawakabili washtakiwa wote, inadaiwa kati ya Aprili mosi, mwaka 2019 na Desemba 31, 2020 maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam waliandaa genge la uhalifu wakajipatia kwa udanganyifu Sh. 4,786,800,000 katika Benki ya NBC tawi la Mnazimmoja.

Alidai, shkata la pili linawakabili washtakiwa wote, wanadaiwa kusababisha hasara, katika kipindi hicho kwa nia ovu waliisababishia Benki ya NBC hasara ya Sh. 4,786,800,000.

Shtaka la tatu, washtakiwa wote wanadaiwa walitakatisha Sh. bilioni 4.78 wakati wakijua fedha hizo ni zao la kosa la kughushi.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 371 ya kughushi nyaraka mbalimbali zikiwamo za Benki ya NBC na mkataba wa udhamini na barua ya Bodi ya Wadhamini wakionyesha kwamba bodi hiyo inawatambulisha watumishi kuwa ni wafanyakazi wa kudumu wa Kampuni ya Peertech.

Watuhumiwa wanadaiwa kudanganya kwamba wafanyakazi 78 wa Kampuni ya Peertech ni wa kudumu na kampuni hiyo imewadhamini wapewe mkopo wa Sh. 4,786,800,000 na Benki ya NBC wakati ni uongo.

Wakili Nguka anadai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka mengine 371 ya kuwasilisha nyaraka za uongo Benki ya NBC Masaki huku wakijua zimeghushiwa.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu lolote sababu Mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri la Uhujumu Uchumi hadi itakapopewa kibali.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi uko katika hatua ya mwisho kukamilika, wanatarajia kuwasilisha taarifa Mahakama Kuu na waliomba Mahakama ihamie Hospitali ya Kitengule kwa ajili ya kumsomea mashtaka mshtakiwa wa tisa, Paul Shayo.

Hakimu Tarimo, aliahirisha kesi hiyo hadi Aprili 13, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa. Mshtakiwa wa tisa alisomewa mashtaka hayo kitandani, wengine walirudishwa rumande.



## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED
## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

1st Housing

**Imetolewa chini ya kanuni ya 58 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Mikopo ya Nyumba) ya Mwaka 2015.**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2021 | Mwaka uliopita 31st Dec. 2020 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 615 | 2 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,601,639 | 2,542,147 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 945,171 | 8,921,407 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 13,570,278 | 6,254,136 |
| 12 | Mali Nyingine | 575,929 | 585,857 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 449,612 | 247,025 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **20,765,244** | **20,172,574** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 488,087 | 413,087 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,008,249 | 723,747 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 41,070 | 41,070 |
| 27 | Dhima Nyingine | - | - |
| 28 | Madeni | 1,010,685 | 1,010,479 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **2,548,091** | **2,188,383** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **18,217,153** | **17,984,191** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,911,640) | (3,424,069) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 232,962 | (487,571) |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **38** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,217,153** | **17,984,191** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 329,009 | 135,854 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 55,648 | 55,828 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 87.73% | 89.15% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.39% | 2.16% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 2825.75% | 1525.46% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65.35% | 31.00% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88.34% | 82.06% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 18.16% | 0.00% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.94% | 1.54% |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| **Jina na Cheo :** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | **(Imesainiwa)** | **30.03.2022** |
| Amulike Kamwela **(Ofisa Mkuu wa Fedha)** | **(Imesainiwa)** | **30.03.2022** |
| Isambo Binde **(Meneja - Mkaguzi wa Ndani)** | **(Imesainiwa)** | **30.03.2022** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| S/No | Maelezo | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2021 | Mwaka Uliopita 31st Dec. 2020 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,487,835 | 1,611,080 |
| 2 | Gharama za Riba | (122,779) | (35,911) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **2,365,056** | **1,575,169** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (17,041) | 47,524 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **130,606** | **24,001** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (1,464) | (2,622) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 53,781 | 7,650 |
| | 6.3 Gawio | 35,130 | 10,333 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 43,159 | 8,640 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(2,229,229)** | **(2,125,095)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,165,923) | (947,092) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,063,306) | (1,178,003) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **249,392** | **(478,401)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (16,430) | (9,170) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **232,962** | **(487,571)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **232,962** | **(487,571)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 19 | 12 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 1.07 | (2.24) |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 |
| | | | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.12% | -2.44% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.28% | -2.67% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 89.32% | 129.97% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 12.89% | 9.33% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa (2021)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 21,800,000 | - | (3,911,640) | - | - | 95,831 | 17,984,191 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 232,962 | - | - | - | 232,962 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (24,348) | 24,348 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 21,800,000 | - | (3,703,026) | 24,348 | - | 95,831 | 18,217,153 |
| | | | | | | | |
| **Mwaka uliopita (2020)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 21,800,000 | - | (3,424,069) | - | - | 95,831 | 18,471,762 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (487,571) | - | - | - | (487,571) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 21,800,000 | - | (3,911,640) | - | - | 95,831 | 17,984,191 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| **Jina:** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| **Vinod Rustagi** Mkurugenzi | **(Imesainiwa)** | **30.03.2022** |
| **Jackson Lohay** Mkurugenzi | **(Imesainiwa)** | **30.03.2022** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| S/No | | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2021 | Mwaka Uliopita 31st Dec. 2020 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **249,392** | **(478,401)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 321,866 | 517,159 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (7,376,039) | (4,213,845) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 75,000 | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (50,276) | (60,932) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (44,042) | (73,121) |
| | - Kodi iliyolipwa | (12,917) | (8,137) |
| | - Mengineyo | (5,640) | (11,748) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(6,842,656)** | **(4,329,025)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | 35,130 | 10,627 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (48,243) | (11,828) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (1,059,492) | (2,542,147) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | (2,028) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,072,605)** | **(2,545,376)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Ulipaji wa deni la Lease Liability | (95,154) | (146,222) |
| | Mengineyo (Mkopo kutoka TMRC) | - | 1,000,000 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(95,154)** | **853,778** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na** | **(8,010,415)** | **(6,020,623)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka | 8,921,409 | 14,894,049 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | 34,792 | 47,983 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **945,786** | **8,921,409** |

1st Housing
Homes within your reach

Unlike banks we aren't limited to options when it comes to Home Loans.

Being a dedicated mortgage provider, we have a variety of products on home loans which can be cherry picked for every individual.



THE MORTGAGE FINANCIAL INSTITUTION
Dar es Salaam
Plot No. 19, Barack Obama Drive | Postal Address 11990 | +255 22 2113456 |
info@firsthousing.co.tz | www.firsthousing.co.tz

216784302

# Marubani waliookoa watu 80 kupewa zawadi maalum

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi inatarajia kuwapa zawadi maalumu marubani wawili waliookoa maisha ya watu zaidi ya 80 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (KIA) kwa kuheshimu jitihada zao walizoonyesha wakati wakilitumikia taifa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Gabriel Migire, alibainisha hayo jana mjini hapa alipotoa tuzo kwa wafanyakazi bora 14 kwenye kikao cha pili cha Baraza la Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

Migire alisema ATCL inapaswa kupongezwa kwa kutambua mchango wa marubani hao katika umahiri wao kwenye kazi, jambo ambalo serikali nayo imelitambua na inajipanga kufanya jambo juu ya marubani hao.

Aliwataja marubani hao kuwa ni Alexander Morgan aliyekuwa rubani msaidizi na Suhad Soud Khasim aliyekuwa rubani mkuu waliokuwa wakiendesha ndege aina ya AirBus yenye namba za usajili TC 110 iliyokuwa ikiruka kutoka KIA kwenda jijini Dar es Salaam mnamo mwaka 2020.

Alisema wakati ndege hiyo ikiwa katika hatua ya kuruka, walimwona mnyama ambaye hakufahamika, kwa haraka akikatisha eneo la njia ya ndege, jambo lililosababisha rubani kutumia jitihada mbalimbali kuzuia ndege isiendelee mbele na ilisimama.

Katibu Mkuu huyo alisema ndege hiyo ilibeba wananchi wakiwamo viongozi mbalimbali wakiwamo wa chama na serikali ambapo kama ndege hiyo ingeendelea na safari ni wazi kwama kungetokea ajali mbaya na kuua idadi kubwa ya watu.

Migire alipongeza ATCL kwa jitihada zake katika kazi na kuleta mafanikio licha ya kutikiswa na ugonjwa wa UVIKO-19 miaka mitatu iliyopita.

Alisema mafanikio ya ATCL yanaonekana kupitia wizara na idara zingine ikiwamo utalii, sekta inayoshika nafasi za juu katika kukuza uchumi na kuboresha uchangiaji wa Pato la Taifa.

Aliwataka watumishi wa ATCL kuitambua nafasi yao kwenye serikali katika kukuza uchumi wa nchi huku wakijipanga kufanya mambo mazuri ikiwamo kuwa waadilifu na wabunifu wa mambo mbalimbali.

"ATCL ni taasisi muhimu kwa serikali, ipo katika maeneo matatu muhimu ambayo serikali haiachi kuzungumzia na kuyapa vipaumbele katika mambo mbalimbali ikiwamo mradi wa reli- SGR, wa umeme - Bwawa la Nyerere na ya tatu ni ATCL.

"Sasa ATCL imetengewa bajeti kubwa ya Sh. bilioni 450 na kuongezewa hadi kufikia Sh. bilioni 640 ambapo kama tutafanya vibaya, ni wazi tutajulikana," alionya.

Mwenyekiti wa Baraza la ATCL, Ladislaus Matindi, alisema kwa kuzingatia kaulimbiu ya baraza hilo ya "Zingatia Taratibu, Tufanikiwe', inawapa mwelekeo unaohitajika baada ya kufanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa kuweka miundombinu, mifumo na taratibu zinazohitajika.

Mmoja wa waliopewa tuzo na ATCL, Mhasibu Julieth Kemanjo, alisema alifanya kazi kwa kujituma na hivyo jitihada zake kumfikisha kwenye mafanikio hayo, akiwahamasisha watumishi wenzake kujituma badala ya kusubiri kutumwa.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Nehemiah Mchechu, ofisini kwake jijini Dodoma, jana. **PICHA: NHC**

# Mtaka ataka NHC kuendeleza jiji la Dodoma

**Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameliomba Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwekeza zaidi jijini humo kwa kujenga nyumba na majengo makubwa ya biashara ambayo yatabadilisha mwonekano wa sasa.

Pia amesema imani kubwa na utendaji kazi wa Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Nehemiah Mchechu, hivyo ni wazi kwamba Jiji la Dodoma litabadilika kwa kuwa majengo makubwa ambayo yatajengwa yatasaidia kulifanya kuwa la kisasa zaidi.

Mtaka aliyasema hayo jana alipokutana na Mchechu na kubadilisha naye uzoefu kwa ajili ya uendelezaji wa jiji la Dodoma.

Alisema hatua ya serikali kuhamishia makao makuu Dodoma ni dhahiri kuwa jiji la Dodoma linahitaji kubadilika kwa kuwa na majengo makubwa ya kisasa ambayo yatasaidia kukuza uchumi wa nchi na kuonyesha uhalisia wa jiji.

"Mchechu nina imani kubwa sana na wewe katika masuala ya ubunifu na uendelezaji miji. Nikuombe sasa ufikirie kulibadilisha jiji hili kwa kutujengea majengo makubwa ya kisasa ambayo yatalipa hadhi jiji letu. Kwa sasa jiji limekuwa na wageni wengi wakubwa wa kimataifa ambao wanafika hapa," alisema Mtaka. Alisema Kamati ya Ujenzi ya Jiji pamoja na wote wanaohusika na masuala ya uendelezaji wa jiji wako tayari kushirikiana na NHC katika kuhakikisha Dodoma ya leo inakuwa mpya zaidi.

Mtaka alisema lengo ni kuitumia ardhi iliyopo vizuri kwa kujenga majengo makubwa ya biashara na nyumba za makazi ambazo zitaendana na hadhi ya makao makuu ya nchi.

"Miji ya wenzetu imeendelea sana na hata ile ambayo imehamisha makao makuu ya nchi zao pembezoni mwa miji ikiwamo Abuja imebaidilisha kabisa mandhari ya miji hiyo na kuifanya kuwa ya kisasa zaidi.

Ni imani kuwa hata sisi Tanzania tunaweza. NHC tumieni fursa hiyo," alisisitiza.

Mchechu kwa upande wake alimshukuru Mtaka kwa imani aliyo nayo kwake na shirika kwa ujumla na kuahidi kuwa ataitumia fursa aliyompatia katika kuliendeleza jiji la Dodoma.

Mkurugenzi Mkuu huyo aliahidi kuwa wiki ijayo atarudi tena Dodoma, hivyo atatumia fursa hiyo kukutana na uongozi ili kuona ni kwa namna gani wanaweza kushirikina katika kuendeleza jiji la Dodoma.



## Balozi Ole Naiko afariki dunia Dar

**Na Jenifer Gilla**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Balozi Emannuel Ole Naiko, amefariki dunia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na familia yake, kifo cha baba yao kilitokea jana nyumbani kwake Bahari Beach mkoani Dar es Salaam.

Balozi Ole Naiko amewahi kushika nyadhifa mbalimbali serikalini mbali na kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TIC. Wakati umauti unamfika, alikuwa ni Balozi wa Heshima wa Botswana.

Taarifa ya familia ilibainisha kuwa mipango ya mazishi inaendelea nyumbani kwake Utulivu Road, Bahari Beach, Dar es Salaam.

## RC ahimiza vijana chanjo UVIKO-19

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, amewataka vijana mkoani Njombe kupata chanjo ya UVIKO-19 na kufanya mazoezi ili afya zao ziweze kuwa salama.

Kindamba aliyasema hayo wakati akizungumza na vijana 200 waliochaguliwa katika uandikishaji anuani za makazi na kueleza hakuna ukweli wowote kwamba chanjo hiyo sio salama.

"Chanjo hii ni salama nawaombeni vijana mkachanje ili muwe salama, vijana msikae burebure mfanye mazoezi ni muhimu nyinyi ni mtaji kwa taifa. Pia, nawaomba mkawe mabalozi wazuri wa zoezi la anuani za makazi na kuwaambia wananchi umuhimu wa chanjo," alisema Kindamba.

Alisema amefanya mazungumzo na viongozi wa dini mkoani humo ili kila nyumba ya ibada ipatikane huduma ya chanjo hiyo.

"Nimeongea na viongozi wa dini kwamba kila siku za ibada wawe wanatoa elimu ya chanjo ya Uviko-19 na kuweka mahema ya chanjo nje ya makanisa na misikiti ili kila mwananchi aweze kuchanja," alisema Kindamba.

Hata hivyo, Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Abdullah Hassan Mwingi, alisema chanjo hiyo ni hiari, lakini kwa chama hicho ni lazima watu wakachanje.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alitoa rai kwa wananchi wa halmashauri ya mji wa Njombe kutoa ushirikiano kwa vijana hao ili kufanya kwa ufanisi.

"Nitoe rai wananchi mjini Njombe kutoa ushirikiano kwa vijana hawa, sio akifika katika nyumba yako umfukuze au umwambie lugha mbaya hii itakua sio sawa, kwa sababu zoezi hili ni muhimu kulingana na kukua kwa teknolojia ," alisema Kissa.

Naye Katibu Tawala, Wilaya ya Njombe, Emmanuel George, aliwataka vijana hao kufanya kazi kwa kufuata maadili na uzalendo ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji Njombe, Kuluthumu Sadick, alisema ana imani na vijana hao na kwamba watakwenda kufanya zoezi hilo kwa umakini na haraka ili kuleta tija.

# LITA yatakiwa kutoa elimu ya mifugo

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo, Tixon Nzunda, ameutaka Wakala wa Elimu ya Mafunzo ya Mifugo nchini (LITA) kuhakikisha inatoa elimu bora ya mifugo ndani na nje ya nchi.

Nzunda aliyasema hayo jijini Dodoma wakati akifungua kikao cha tisa cha Baraza Kuu la Wafanyakazi la LITA na kuwataka kuwa chanzo cha kuwashauri wafugaji na kutoa maarifa kwa wadau wa sekta ya mifugo ili sekta hiyo iweze kuimarika na kuwa ya kisasa zaidi.

Alisema wakufunzi wa LITA wanatakiwa kuwa chanzo cha kuandaa majarida mbalimbali vikiwamo vitabu vya ufugaji na kupatikana kwa maarifa mapya yanayotokana na utafiti zinazofanywa na wakufunzi hao.

Aidha, alisema wajibu wake ni kuwa karibu na umma kwa kutoa huduma bora ikiwamo ya wanafunzi wanaohitimu kuwa bora na wanaoheshimika, kutambulika, wenye maarifa, wanajiamini na kuandaliwa vizuri kwenda kusaidia sekta binafsi.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi la LITA, Dk. Pius Mwambene, alisema baraza hilo limeendelea kuimarisha uhusiano na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha inaboresha miundombinu ya kufundishia.

Dk. Mwambene alisema kwa sasa wakala huo unakaribia kukamilisha makubaliano ya ujenzi wa kampasi ya LITA mkoani Songwe ikiwa ni jitihada za kuongeza wigo wa elimu ya mifugo katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema katika kuhakikisha wafugaji wanapata mwongozo wa ufugaji bora imeanisha utaratibu wa kuwashikiza wanafunzi wa hatua ya nne kwa wafugaji katika maeneo yao wakati wa likizo ili kuanza kujenga uzoefu ujasiri wa kuwahudumia wafugaji mapema.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angello Mwilawa, alisema wataendelea kusimamia maadili na weledi kwa wafanyakazi na kuongeza ushirikishwaji ili kuwapo na matokeo makubwa yenye maslahi mapana yatakayoleta tija.

Dk. Mwilawa alisema nguvu zaidi zitaelekezwa kwenye maeneo ambayo yatagusa jamii na maelekezo yote yatafanyiwa kazi ili kuongeza ufanisi.

Baadhi ya wajumbe wa baraza katika kikao hicho, wametoa maependekezo kadhaa ya kuboresha utendaji kazi pamoja na mazingira ya wafanyakazi ili waweze kufanya kazi kwa morali na kufikia malengo.

# DAWASA, TANESCO zaagizwa kuwatatulia vikwazo wawekezaji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, ameiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha wanakutana na uongozi wa kiwanda cha kutengeneza chakula cha mifugo kuzalisha vifaranga na mayai.

Sara alitoa maelekezo hayo jana katika ziara yake ya siku moja ya kutembelea viwanda kuona hali ya uzalishaji kwa wawekezaji, na kusikiliza vikwazo wanavyokumbana navyo na kuzitafutia ufumbuzi kwa pamoja.

Alisema lengo la serikali ni kuhakkiisha wawekezaji wanafikia malengo yao, hivyo vikwazo vinavyoelezwa ni lazima vishughulikiwe kwa wakati na uzalishaji uendelee.

"DAWASA wanatakiwa kuona namna ya kuunganisha maji katika kiwanda hiki, kutaneni na mfanye tathmini ni namna gani mnaweza kuunganisha maji hapa na kumaliza kikwazo hiki, kwani wenye mradi kama huu maji lazima yanahitajika mengi," alisema.

Pia aliielekeza TANESCO kuwatembelea wawekezaji wa viwanda kusikiliza vikwazo vyao na wavitafutie ufumbuzi kwa haraka ili shughuli za uzalishaji ziendelee.

Alisema kutokana na maeneo mengine kuelezwa kuwa na miundombinu ya umeme chakavu, ukarabati wa mara kwa mara ufanyike kupunguza adha ya kukatika umeme mara kwa mara.

Akitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya, mwakilishi wa Kiwanda cha Animal Care Company (ACC), Idd Nasibu, alisema wameshatoa ajira 225, na kwamba bidhaa zao wanasambaza katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Tanga na Zanzibar lengo lao ni kufikia nchi nzima.

Alieleza pia vikwazo wavyokumbana navyo ni barabara, umeme usio wa uhakika na maji ya DAWASA.

Nasibu aliwataka vijana kujikita katika shughuli za ufugaji ambazo zinaweza kuwainua kiuchumi badala ya kuendelea kuona kazi sahihi ni kuendesha bodaboda pekee.

Alisema ufugaji ni sehemu ya ajira ambayo vijana wakijikita huko wanaweza kunufaika zaidi badala ya kusimamia eneo la bodaboda, ambalo baadhi yao wameliona ni sehemu ya ajira zao baada ya kukosa sehemu nyingine.

Katika kiwanda cha pamba za kutengenezea mito na magodoro, walieleza uhaba wa malighafi ya chupa za maji, hali inayosababisha kuzalisha chini ya kiwango.



NaibuKamishnawaMamlakayaUdhibitiwaBima Tanzania (TIRA), Khadija Issa Said (wapilikulia), akimkabidhimfanowaBimaKamilifuyaBiasharanagari Mkurugenziwa LPG, Laura Johnson, wakatiwahaflayaWanawakenaBima, jijini Dar es Salaam jana. WengineniOfisaMtendajiMkuuwaKampuniya Fortis Insurance Brokers, Maryam Shamo (kulia),OfisaMtendajiMkuuwaKampuniyaLilian Production Group (LPG), LilianMyaka (wapilikushoto) naMenejaMkuuwa Assemble Insurance, TabiaMassudi. BimahiyoimetolewanaKampuniya Fortis kuhamasishawadauwatambueumuhimuwahudumazabima. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yaombwa kuanzisha vituo vya malezi na makuzi

**Na Happy Severine,** MASWA

SERIKALI kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeombwa kuanzisha vituo vya malezi na makuzi ya awali kwa watoto wenye umri kati ya miaka mitatu hadi minne ikiwa ni moja ya mikakati ya kumjenga na kumlinda mtoto.

Hayo yameelezwa jana wilayani hapa na baadhi ya wazazi na walezi wa wanafunzi katika vituo vya malezi na makuzi ya awali ya mtoto vya Kasajo Day Care na St. Josephine Bhakita, wakati wakizungumza na waandishi wa habari waliotembelea vituo hivyo kwa nyakati tofauti.

Walisema kuwa vituo vya malezi na makuzi kwa watoto ni muhimu ili kuhakikisha watoto wanapata huduma bora zitakazowezesha uchechemuzi wa bongo zao na kuwekwa katika mazingira mazuri ya ukuaji.

"Hivi ni vituo muhimu unaweza ukadhani ni jambo dogo, hili ni jambo kubwa sana na la msingi katika malezi na makuzi ya awali kwa watoto wetu," alisema Janeth John.

Walisema kuwa vituo hivyo ni suluhisho tosha kwa tatizo la malezi na makuzi ya mtoto hasa kwa changamoto za utafutaji kipato kwa wazazi kukosa muda mwingi wa asubuhi mpaka jioni kukaa na watoto wao.

"Vituo vya malezi na makuzi ya awali kwa watoto vinalenga kutoa fursa kwa wazazi na walezi kutekeleza shughuli za kiuchumi," alisema George Nyagawa. Mkuu wa kituo cha malezi na makuzi cha Lusajo, Edward Khija, alisema kuwa kituo hicho kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018 mpaka 2020 kimefanikiwa kuwaandaa watoto zaidi ya 200 kabla ya kuwapeleka katika shule za awali.

"Walimu katika shule tulizowapeleka watoto hao wanasema wanaopitia katika kituo hiki wanakuwa na uelewa wa haraka ikilinganishwa na ambao hawajapitia katika vituo vya malezi," alisema.

Aliongeza kuwa ujifunzaji kwa watoto umezingatia falsafa za malezi na makuzi ya mtoto zinazohimiza umuhimu wa miaka ya mwanzo ya mtoto kupata uangalizi na malezi bora kwa kuwa ni msingi wa maisha ya baadaye.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, alisema kwa umuhimu wa vituo vya malezi na makuzi ya mtoto ni vizuri taasisi binafsi na za madhehebu ya dini kuanzisha vituo hivyo ambavyo kwa sasa vina umuhinu mkubwa katika jamii.

"Kwa mfumo wa serikali elimu inaanzia elimu ya awali hadi chuo kikuu hivyo ni vizuri kwa jamii hasa sekta binafsi yakiwamo madhehebu ya dini yakaanzisha vituo hivyo na serikali ni lazima itoe miongozo ya utoaji wa elimu hiyo ambayo ni muhimu kwa kumwandaa mtoto kuingia shule ya awali na msingi," alisema.

# Serikali yaipa maelekezo DP World

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imeitaka kampuni ya usafirishaji wa mizigo ya DP World iliyoingia makubaliano na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) kuhakikisha usalama wa mali za wateja unazingatiwa wanapoagiza bidhaa zao kwa njia ya mtandao.

Maelekezo hayo yalitolewa Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara, wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Biashara za jumla mtandaoni unaojulikana kwa jina la Dubuy. Com Tanzania.

Kampuni ya DP World na TCCIA iliwekeana saini ya makubaliano kati ya taasisi hizo mbili kwa kufungua ukanda mpya wa biashara ya kidigitali nchini na ukanda wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kutoa fursa kwa Watanzania kushiriki katika masoko ya nje.

Prof. Kahyarara alisema mkataba huo ni matunda ya maonyesho ya kimataifa ya Dubai Expo ambapo Tanzania ilikuwa mshiriki.

Alisema maonyesho ya Dubai Expo yamezaa matunda na makubaliano hayo yaliyofanyika ni muhimu hasa katika biashara za mtandao inarahisisha ufanyaji wa biashara na mteja kupata bidhaa kwa wakati.

Aidha, alisema wakati wakiwa Dubai walisaini mikataba 36 mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan na siku iliyofuata ukaongezeka mkataba mwingine na kufikia 37 na yote ni kwa ajili ya biashara na uwekezaji.

"Mpaka sasa hivi katika miradi hiyo 37 ilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani bilioni nane sawa na zaidi ya Sh. trilioni 16 huu umeongezeka kutokana na matokeo ya Dubai Expo ndio maana tumekuja kushuhudia," alisema.

Alisema mpaka sasa wana mikataba 38 na hatua itakayofuata watafanya tathmini kuangalia utakuwa una thamani gani ya kiuchumi ili kuongezea gharama katika hesabu walizofanya awali ya Dola za Kimarekani bilioni nane.

Alishukuru kampuni ya DP World kwa kuja nchini kuwasaidia katika kufungua fursa za uwekezaji, kibiashara na kufanya biashara katika dunia ya leo ya matumizi ya mtandao.

"Nawapongeza na wenzetu wa TCCIA kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, tunaimani itasaidia katika kuongeza utendaji wa kibiashara na sekta binafsi katika kufikia masoko ya nje."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dubai Trade Word, Mohamood Al Bastaki, alisema Dubuy. com inatoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani kukua na kufikia kiwango cha kimataifa kwa kuwawezesha kushiriki katika masoko mapya barani Afrika, mashariki ya kati na maeneo mengine duniani.

Alisema uzinduzi wa jukwaa hili Tanzania ni soko muhimu na itasaidia katika ukuaji wa uchumi na fursa za biashara mtandaoni ambazo kwa muda mrefu hazijatumiwa ipasavyo.

Naye Rais wa TCCIA, Paul Koyi, alisema Dira ya Maendeleo ya Tanzania kufikia mwaka 2025 ni kuwa na uchumi imara, mtambuka, unaostahili ushindani ambao unaendana na mabadiliko ya teknolojia.




Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akizungumza katika mkutano wa uzinduzi wa ripoti ya uwekezaji kutoka Umoja wa Ulaya (EU) nchini, jijini Dar es Salaam jana, inayolenga kuchangia ukuaji na maendeleo kwenye sekta za kilimo, viwanda, utalii na madini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi VETA watajwa ni mkombozi wakazi Mafia

**Na Mary Geofrey,** MAFIA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, amesema kukamilika kwa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kisiwani Mafia kutatoa ujuzi kwa vijana katika fani za uvuvi, udereva na utalii.

Alisema juzi kisiwani hapa kwamba taaluma hizo zitawasaidia wakazi wa kisiwa hicho ambao kwa asilimia kubwa wanajihusha na shughuli za uvuvi, kujiendeleza na kuongeza thamani ya mazao na kukuza uchumi wao na wilaya kwa ujumla.

Kipanga, alipotembelea juzi chuo hicho cha Nagondi, alisema: "Ujenzi ukikamilika vijana wetu watajifunza namna ya kuvua salama kitaalamu na kuchakata mazao ya baharini likiwamo zao samaki na mwani."

Alisema chuo hicho pia kitafundisha udereva wa magari na pikipiki kwa vijana wa wilaya hiyo kwa kuwa hawajawahi kupata elimu ya udereva na hawana leseni za kuendesha pikipiki.

"Leseni wanazifuata wilayani Kibaha, kunawagharimu hadi Sh. 300,000 kufuatilia na ndiyo sababu wanaona hakuna umuhimu wa kuwa nazo, hivyo uwapo wa chuo hiki ni mkombozi mkubwa," alisema Kipanga.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Wilaya hiyo kusimamia ujenzi huo ukamilike ndani ya mwezi mmoja ili vijana wa wilaya hiyo waanze kunufaika.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Martin Ntemo, alisema wilaya hiyo ina wakazi 52,000 na asilimia 70 ya makusanyo ya wilaya hiyo yanatokana na shughuli ya uvuvi zinazofanywa na watu wa rika lote.

Makamu Mkuu wa Chuo cha VETA Mkoa wa Lindi, Allyse Mmari, anayesimamia ujenzi huo, alisema majengo 17 yamejengwa na baada ya kukamilika, wanafunzi 720 watanufaika wakiwamo 240 wa kozi za muda mrefu na 480 za muda mfupi.

Alisema ujenzi wake umefika asilimia 70 na gharama za ujenzi wa mradi huo ni Sh. bilioni 2.8 na ukikamilika utanufaisha wananchi wa wilaya hiyo hususani vijana.

# Moro kuwa kitovu uzalishaji chakula

**Mwandishi Wetu,** MOROGORO

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kwa ushirikiano na mashirika ya kimataifa yanayolinda wanyamapori na mazingira yanasimamia mikutano mitatu kila siku kuanzia Jumanne hadi leo.

Maoni ya mikutano hiyo yatasaidia kuandaa mpango kazi wa kutekeleza maazimio ya mkutano wa siku mbili uliofanyika katikati ya mwezi huu ambayo yanayolenga kuifanya Morogoro kitovu muhimu cha uzalishaji katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi. Kwa sasa msisitizo unawekwa kwenye Wilaya ya Kilombero.

Mwenyekiti wa Kundi la Mashirika yasiyo Kiserikali katika mkutano uliopita, Alexander Mpwaga, alisema jana kwamba sekta binafsi inakutana leo na kuchambua masuala yanayotokana na maazimio hayo, kesho watoa huduma watakutana kwa lengo hilo hilo na Alhamisi wawakilishi wa makundi hayo watakutana na viongozi wa serikali ya mkoa wa Morogoro.

"Maazimio ya mkutano wetu yatatekelezwa kulingana na mpango kazi. Kwa hiyo SAGCOT inashirikiana na World Wildlife Fund (WWF) na African Wildlife Foundation (AWF) katika kuandaa mikutano hiyo mitatu ambayo itatoa maoni ya kuwezesha kuandaliwa kwa mpango kazi huo, alieleza Mpwaga.

Katikati ya mwezi uliopita SAGCOT kwa ushirikiano na serikali ya Mkoa wa Morogoro iliandaa mkutano uliowakutanisha mabingwa 170 kutoka katika sekta za binafsi, sekta ya umma na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambao ulijadili namna ya kuingiza uzalishaji wa kisasa katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika Mkoa wa Morogoro na hasa Wilaya ya Kilombero.

Majadiliano hayo ya siku mbili yalihitimishwa kwa kusaini makubaliano ya kujenga sekta ya kilimo ambayo ni ya kibiashara katika Kongani ya Kilombero (au Mkoa wa Morogoro) kwa lengo la kuendeleza usalama wa chakula, kuinua hali na kipato cha wakulima na kuhakikisha mazingira yanabaki endelevu.

Mkutano huo, uliotoa maazimio na mapendekezo ya kuondoa vikwazo katika kilimo, ulihusisha watumishi wa serikali, sekta binafsi na watoa huduma (au mashirika yasiyo ya kiserikali), jumuiya ya wasomi (academia) na vyama vya vikuu ya wananchi (apex organizations) vinavyofanyakazi katika Mkoa wa Morogoro.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela ambaye aliahidi kwamba serikali kwa upande wake itafanya kila linalowezekana kutekeleza makubaliano na maazimio ya mkutano huo.

Mpwaga, ambaye ni mshauri wa kilimo na Mwenyekiti wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika Wilaya ya Kilombero, alisema mikutano hii ni kielelezo cha mwanzo mzuri wa utekelezaji wa maazimio ya mkutano uliopita.

ama
ALHAMISI MACHI 31, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**ELIMU KWA WACHIMBAJI WADOGO ...**
**Serikali imeamua kushughulikia shida ya utumiaji baruti na watoto migodini**



Ukurasa 12

**Wanamichezo wakombozi wapya wa afya wachangia damu, huduma**

# Covid- 19 ilivyokuja na changamoto yake kwa watoto wenye kifafa

**Na Jenifer Gilla**

NI saa tisa alasiri, Latifa Iddy (29) anashtuka kutoka usingizini na kumwangalia mwanaye mwenye umri wa miaka mitatu, aliyekuwa amelala ubavuni mwake.

Hofu inamtanda na anajikuta anamuita mama yake (bibi wa mtoto) kwa sauti "mamaa, maamaa njoo haraka mtoto amepata degedege tena".

Kinachomshangaza mama wa mtoto huyo, ni kuwa amepata degedege kwa mara ya tatu ndani ya siku moja, hali ambayo si ya kawaida. Latifa anafafanua:

"Alikuwa na homa na mafua na tulimpa dawa lakini cha kushangaza akapata degedege mara 3 kwa siku moja, hali ambayo haijawahi kutokea tangu apate ugonjwa huo akiwa na umri wa miezi sita."

Akiwa mwenye hofu na mwili mzima unamtiririka jasho, alimbeba mwanawe mgongoni akakimbilia Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) , anakohudhuria kliniki ya mtoto huyo, kwa aliyoyakuta yanamstaajabisha zaidi.

"Kufika hospitali nikakuta wazazi wenzangu wanne ambao nao watoto wao wanaanguka zaidi ya mara moja kwa siku kama wa kwangu, ndipo tukaingia kwa daktari akatuambia kuwa kwa sasa kuna homa kali ambazo husababisha tatizo hilo kwa wagonjwa wa kifafa," anasimulia.

Fides Uiso (34) mama wa mtoto wa miaka mitano, anasimulia mwanawe alipata mafua makali kwa siku mbili, ikawa chanzo chake kupata degedege mara mbili kwa siku, hata kumtia hofu akidhani kuna tatizo kubwa.



Mtaalamu wa magonjwa ya mfumo wa fahamu na ubongo kwa watoto wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Edward Kija. **PICHA: JENIFER GILA**

"Alipata mafua makali siku tatu mfululizo, ile siku ya mwisho alipata degedege asubuhi na jioni na siku ya nne pia asubuhi akaugua, ndipo nikaona hapa lazima niende hospitali pengine mwanangu ugonjwa umekuwa sugu," anasimulia Fides kwa uchungu.

Mtaalamu wa Magonjwa ya Mfumo wa Fahamu na Ubongo kwa Watoto, Muhimbili, Dk. Edward Kija, anakiri kuwapo ongezeko la watoto wenye kifafa kilichodhibitiwa. Pia, kuanguka degedege kila mara kunatokana na homa pia mafua makali kipindi cha mlipuko wa Covid-19.

"Kwa kawaida mgonjwa mwenye kifafa ambaye anakunywa dawa zake vizuri, huwa haanguki degedege. Maana yake ni kifafa kimedhibitwa, isipokuwa kama atapata 'infection' (athari) za bakteria au virusi ambavyo humletea homa, mafua au kifua, ndipo atapata degedege ila akitumia dawa anakaa sawa," anasema Dk Kije.

Anaendelea: "Kipindi ambacho ugonjwa wa Covid-19 unaingia, kulikuwapo homa na mafua makali ambayo yaliwapata hadi watoto, Sasa hawa wenye ugonjwa wa kifafa ndio wakawa wanapata degedege zaidi ya mara moja kwa siku kutokana na homa kuwa kali," anafafanua

**WALIVYOUTIBU**

Mtaalamu huyo anasema walikuwa wakitoa dawa za kusitisha degedege kwa mgonjwa ili apewe matibabu mengine.

"Tulikuwa tunampima mgonjwa kuangalia nini kimesababisha kupata degedege. Kama ana homa kali basi tutampa dawa za kushusha homa na kama ana mafua tulimwandikia dawa na tunashukuru Mungu tulipata matokeo mazuri, " anasema.

Daktari Kija, anasema walipobaini huenda hali imesababishwa na wimbi la Covid -19, wakatoa elimu kwa wazazi namna ilivyo uhusiano baina ya virusi hivyo na ugonjwa wa kifafa, ili wachukue tahadhari.

Dk Jaqueline French, mtaalam wa ugonjwa wa kifafa kutoka asasi ya Epilepsy Foundation, anasema wenye kifafa wapo hatarini kuambukizwa Covid-19, kutokana na sababu mbalimbali.

Mojawapo anataja kuwa, kutumia dawa za kudhibiti kifafa, pia huathiri mfumo wao wa kinga na watoto wenye ugonjwa huo, wapo hatarini kuambukizwa Covid-19.

**WAKIMBIA KLINIKI**

Mlipuko wa Covid 19 unatajwa kuchangia baadhi ya wagonjwa kukwepa mikusanyiko, huku kukiwapo wengi walioacha kuhudhuria kliniki kutokana na maambukizi yake.

Hapo anasema ikazua changamoto ya mahudhurio ya kliniki, huku akilalamika: "Baadhi yao walizidiwa wakiwa nyumbani na waliletwa hapa wakiwa wameathirika zaidi."

Asnath Mashiwa, mama wa mtoto wa miaka miwili, anataja magumu aliyopata ni kumtoa mtoto nyumbani kumpeleka hospitali, hasa ikizingatiwa tahadhari zilihitajika, huku akijiuliza namna ya kuvalisha barakoa.

Katika hilo, akabeba imani hatari ya uhai wa mtoto wake kwa kwenda naye hospitali, huku sura ya pili alijiuliza hatari ya kumuacha mtoto nyumbani, ambayo ndio ikaangukia uamuzi wake, akiamini hospitalini kulikuwa hatari zaidi.

Dk. Kije anasema athari za mtu mwenye kifafa kutotumia dawa ni kuathiri sehemu ya utendaji wa

**Inaendelea Uk. 12**

AFYA

# Wanamichezo wakombozi wapya wa afya wachangia damu, huduma

- Mechi maalum ya kumchangia mtoto
- Watani wahamasika kuchangia damu

**Na Adam Fungamwango**

KWA miaka ya karibuni imeonekana sekta ya Afya ikianza kushirikiana na ya michezo, hali inayozaa matunda na kuleta mafanikio makubwa.

Si ushirikiano rasmi, lakini wadau wa michezo kwa miaka ya karibuni wameonekana kuwa na mwamko mkubwa, hasa wakihamasishwa na viongozi wao kujitolea kuwasaidia wananchi wenzao wahitaji au wagonjwa.

Hiyo inaonyesha kuwa Wizara ya Afya na ile ya Utamaduni, Sanaa na Michezo zitakapokaa na kukubaliana kitu kimoja na klabu kubwa nchini kama Simba na Yanga, basi kuna matarajio kiasi kikubwa nchini damu kuchangiwa.

Hivi karibuni klabu ya Yanga jijini Dar es Salaam, iliandaa mchezo maalum kwa ajili ya kumchangia mtoto Ali Kimara mwenye umri wa miaka 10, ambaye amekuwa akisumbuliwa na changamoto ya upumuaji kwa takribani miaka minane sasa.

Ni mechi iliyochezwa tarehe 12 mwezi huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, kati ya Yanga dhidi ya timu ya Taifa ya Somalia.

Kabla ya mechi hiyo kuanza, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu alipiga simu moja kwa moja, na kuahidi kutoa shilingi milioni 15 kwa taasisi inayomshughulikia mtoto huyo, inayojishughulisha na kuwasemea watoto wote wenye magonjwa adimu yasiyo na tiba.

Ali amekuwa akitumia mashine ya umeme kumsaidia kupumua kwa saa 24 akiwa anawekewa mtungi wa gesi pale umeme unapokatika.

"Suala hili la magonjwa adimu tumehangaika nalo muda sasa, tunafurahi kuona Yanga wamelifikisha kwa umma na mimi kwa kuunga mkono, naahidi kutoa kiasi cha shilingi milioni 15 kuisaidia taasisi hiyo," anasema Rais Samia.

Wengine walioungana kuchangia taasisi hiyo siku hiyo ni taasisi ya GSM iliyotoa shilingi milioni 10.

Akizungumza uwanjani hapo, mama mzazi wa Ali, Sharifa Mbarak, akafafanua lengo la taasisi hiyo ni kuwasemea watoto wenye magonjwa adimu kuwafikia watunga sera, wafanya maamuzi na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na wanavyoumwa.

Hiyo ni baada ya viongozi wa Yanga na mwanasoka wake mahiri Fiston Mayele, kumtembelea nyumbani wao Upanga, Dar es Salaam.

Pia, mwezi huu viongozi, safu ya ufundi na wachezaji wa Yanga waliungana na Watanzania wote kwenye kumbukumbu ya mwaka mmoja wa kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, John Magufuli, kwa kuwatembelea wagonjwa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dar es Salaam.

Pia, wanachama na mashabiki wa Yanga wakajitokeza kwenye Taasisi ya Mifupa (MOI) kuchangia damu.

Mwezi Agosti mwaka jana, viongozi wanachama na mashabiki wa klabu ya Simba, nao walitembelea kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwananyamala kusaidia afya ya mama na mtoto.



Mwana – Yanga, akichangia damu kwa wagonjwa hospitalini.
**PICHA: MTANDAO.**

Hiyo ilikuwa kuelekea kwenye kilele cha hafla yao iitwayo 'Simba Day,' msafara uliongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu, Barbara Gonzalez na wakatoa fedha kiasi cha shilingi milioni 10.

"Uongozi ndiyo unajua kitu gani kinahitajika kwa haraka na kiasi cha fedha tulichotoa kitasaidia sehemu fulani, ingawa tunajua hakitaweza kumaliza kabisa tatizo," akasema Barbara.

Katibu wa hospitali hiyo, Lilian Mwanga, ameupongeza uongozi wa klabu ya Simba kuwasaidia, akitaka uhusiano huo uwe endelevu na akaahidi fedha hizo zitatumika kama zilivyokusudiwa.

"Mnaweza kuona kama ni mdogo, lakini kwetu ni mkubwa na tutaenda kuutumia kama ilivyokusudiwa na tunawakaribisha wakati mwingine," akasema Lilian.

Machi mwaka juzi jumla ya wanachama, wapenzi na mashabiki wa Simba na Yanga 203 walijitokeza kuchangia damu kwenye taasisi ya MOI, kusaidia kuokoa maisha ya majeruhi wa ajali na wanaotibiwa hospitalini.

Mhamasishaji mkubwa kwenye hilo alikuwa mfadhili wa zamani wa Simba, Azim Dewji na zilipatikana jumla ya chupa 187 za damu.

Hiyo ilikuwa kabla ya mechi ya watani wa jadi Simba dhidi ya Yanga iliyochezwa Machi 8, 2020 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, mgeni rasmi alipokuwa Hayati Rais John Magufuli.

Wakati wanachama na mashabiki wa timu hizo wakijitolea damu, Ofisa Habari wa MOI, Patrick Mvungi anasema ni kitendo kinachosaidia kuokoa maisha ya majeruhi wa ajali na wagonjwa wengine wanaohitaji hudumu hiyo.

"Kwa namna ya pekee tunatoa shukrani za dhati kwa Azim Dewji aliyehamasisha na kutoa wito kwa watu binafsi, mashirika, vikundi na asasi kufika MOI kuchangia damu kwa sababu hakuna kiwanda cha damu, bali ni lazima itoke kwa mwili wa biandamu iende kwa mgonjwa," anasema Mvungi.

## Covid- 19 ilivyokuja na changamoto yake kwa watoto wenye kifafa

**Inatoka Uk. 11**

ubongo wake.

"Mtoto mwenye kifafa asipotumia dawa kwa wakati au kucheleweshwa tiba anapata degedege la mara kwa mara ambalo huathiri ubongo," anasema Dk. Mohdraza.

"Ubongo ukiathirika, husababisha baadhi ya viungo kutofanya kazi vizuri kama vile mkono kupinda, kupata utindio wa ubongo," anasema .

Dk. Kija anasema walifanya jitihada kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa corona kwa kutoa dawa za kifafa za muda mrefu,ili kupunguza msongamano wa watu hospitalini.

"Wale waliokuwa na kifafa tulichokidhibiti tuliwapa dawa za kutumia hadi miezi mitatu na tuliwaambia waje hospitalini iwapo mtoto ataugua au vinginevyo," anasema.

Anafafanua ni hali iliyowawezesha kupunguza idadi ya kuona wagonjwa kutoka 70 hadi 20 kwa siku " anasema na kwa waliohofia kufika kuchukua dawa walitumia mbinu mbadala kuwashawishi kujitokeza kuchukua dawa.

Hapo anasema waliwashawishi, angalau mtu mmoja akiwa na tahadhari zote kama kunawa mikono na kuvaa barakoa.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, utaratibu wa kuwaona wagonjwa pia ulibadilika, kwa kupunguza idadi ya wanaofika kuona wagonjwa waliolazwa hospitalini.

Daktari huyo bingwa anasema, kundi la pili ni la wagonjwa wenye degedege ambalo lipo hatarini na wanatakiwa kumuona mtaalam kila siku kwa ajili ya matibabu, akitaja idadi nayo ilipungua. ingawa hakutaja kwa takwimu.

**CHANJO JE?**

Dk Kije anasema, bado hawajaanza kutoa chanjo ya covid -19 kwa watoto kwa kuwa utafiti unaendelea ili kujiridhisha iwapo mtoto wa chini ya miaka 12 anastahili.

Kwa mujibu wa taasisi ya kimataifa ya ugonjwa wa kifafa 'International League Against Epilepsy' hakuna ushahidi unaoashiria kifafa kinachangia athari hasi kwa chanjo ya COVID-19, hasa kuongezeka mshituko.

Hata hivyo, kama zilivyo chanjo nyinginezo, homa inaweza kuzuka baada ya kupokea chanjo ya COVID-19, hata kuchangia matukio ya kuanguka kwa baadhi ya wagonjwa wa kifafa.

Hata hivyo, inatajwa wakitumia dawa za kukabili homa kwa muda wa saa 48 baada ya chanjo au kipindi chote wanachougua homa, hatari inapungua.

**HOFU YA WAZAZI**

Baadhi ya wazazi wameeleza kuwa si tu waliogopa kuwapeleka watoto wao hospitali kuhofia maambukizi ya corona lakini hata kwenye shughuli zao binafsi.

Latifa anaeleza kuwa ilifika wakati alikuwa anaogopa kwenda kazini kwa kuhofia anaweza kupata maambukizi na kumwambukiza mtoto hali iliyoweka kibarua chake hatarini.

"Kuna wakati niliomba ruhusa ya wiki mbili kuangalia hali ya mtoto lakini lengo lilikuwa ni kuepusha kupata maambukizi kwa sababu mtoto alikuwa akipata degedege kila siku na mimi peke yangu ndiye natoka kwenda kazini nikahisi labda mimi ndio namletea mtoto maradhi haya," anasimulia.

Anasema, alitaka kufanya uamuzi wa kuacha kazi lakini akakumbuka kuwa hana mtu wa kumsaidia kifedha kulea mtoto huyo ikabidi aende kazini kwa kuzingatia tahadhari lakini pia alihama chumba anacholala mtoto na akamwacha alale na bibi yake ambaye hatoki nje kama yeye.

Wakati Athnati John (35), aliamua kuacha shughuli ya mama ntilie kwa muda kuhofia kumletea mtoto maambukizi ya ugonjwa huo mpaka pale hali ya maambukizi ilipodhibitiwa ndipo akarudi hali hii ilimsababisha kupoteza wateja wake wote hivyo kulazimika kuanza mwanzo

"Kutokana na kukaa nyumbani miezi mitatu bila kuuza chakula wateja wote walihamia kwa mama ntilie wengine , sasa hivi nimerudi ila siuzi tena chakula kama mama ntilie bali nauza matunda ya msimu," anasimulia.

AFYA

WAKATI AHUENI YATANGAZWA...

# Fahamu inavyotimu miaka miwili ya Uviko 19 nchini na pilika zake

• Kasi maambukizi; wagonjwa 138 hadi watano

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MACHI 16, 2022, Tanzania imetimiza miaka miwili kamili tangu kuthibitika kwa uwepo wa ugonjwa wa virusi vya corona (UVIKO-19) kwa mara ya kwanza hapa nchini.

Katika kipindi chote, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na wanataaluma wa afya na wananchi kwa ujumla imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Hatua ambazo imezichukua kupambana na UVIKO-19 kwa kiasi kikubwa zimezingatia mazingira na hali ya jamii nchini, ikiwamo kuruhusu wananchi kuendelea kujitafutia kipato chao, bila ya kuwa na vikwazo kitaifa.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa UVIKO-19 kwa kipindi cha miaka miwili anasema hadi kufikia Machi 15, 2022, jumla ya watu 33,789 wamethibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO - 19 na watu 803 wamepoteza maisha nchini.

Anasema mikakati iliyotekelezwa na serikali wakati ulipongia ugonjwa huo ni pamoja na kuwaondoa hofu wananchi kuhusu mlipuko wa ugonjwa huo, kufunga shule, vyuo na taasisi za elimu ya juu, kutoa elimu kwa jamii kuhusu kujikinga na ugonjwa .

Pia, ikahimiza jamii kusitisha mikusanyiko isiyokuwa ya lazima, kuimarisha huduma za ukaguzi na uchunguzi wa afya kwa wasafiri katika maeneo ya viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu ili kuzuia kuingia kwa maambukizi nchini na kuboresha mchango wa tiba asili.

"Aidha katika kipindi hiki pia tumeweza kuongeza wigo wa uchunguzi wa kimaabara wa UVIKO-19 ambapo kwa sasa kuna maabara saba ndani ya nchi zenye uwezo wa kupima UVIKO-19 kulinganisha na maabara moja ya Afya ya Jamii iliyokuwepo wakati wa kulipuka kwa ugonjwa huo mwezi Machi 2020.

Anasema maabara hizi ni pamoja na Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii, Maabara katika Hospitali za Kanda za Bugando, Mbeya na Maabara katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Dodoma, Arusha, Kigoma na Maabara iliyopo katika Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

Waziri anasema serikali imesimika mitambo 15 ya hewa tiba ya oksijeni katika hospitali mbalimbali nchini, ili kutoa huduma za wagonjwa mahututi wanaohitaji uangalizi maalum.



Mwananchi Charles Marwa, akipokea cheti cha uthibitisho wa kupata chanjo kutoka kwa Ofisa Muuguzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbli (MNH-Mloganzila), Kanaeli Uriyo, mara baada ya kuchanjwa. **PICHA: MNH.**

Vilevile, anasema hali ya kiwango cha uchanjaji kimikoa ni kama ifuatavyo na asilimia zake kwenye mabano: Ruvuma (23%), Katavi (14%), Dodoma (13%), Mtwara (12%), Mara (11%), Mwanza (11%), Lindi (10%) na Dar-es-Salaam (10%).

Kwingineko ni: Simiyu (10%), Pwani (9), Kilimanjaro (9%), Kagera (9%) na Mbeya (9%) , Arusha (8%), Geita (7%), Shinyanga (7%), Iringa (7%), Njombe (7%), Rukwa (6%), Morogoro (6%), Tanga (5%), Kigoma (5%), Tabora (5%), Singida (5%), Songwe (4%) na Manyara (3%).

Anasema kwa kuzingatia hali hii, mikoa inahitaji kuongeza juhudi katika kuhimiza wananchi kujitokeza kuchanja.

Aidha, anasema kumeonekana kupungua ugonjwa huo kwa sasa hapa nchini ndani ya wiki ya katikati ya mwezi Machi 2022, huku kukiripotiwa taarifa ambazo bado hazijathibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu kuibuka kwa aina mpya ya kirusi cha UVIKO-19 katika nchi za China, South Korea na Japan.

Waziri anafafanua anasema Wizara ya Afya inaendelea kuwasiliana na Shirika la Afya Duniani kuhusu suala hilo sambamba na kuendelea kuimarisha ukaguzi na ufuatilia wa wasafiri wanaoingia nchini kwetu kwa kuimarisha huduma za ukaguzi na uchunguzi wa afya katika maeneo ya viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu.

"Kwa kuzingatia hali ya sasa ya maambukizi ya UVIKO-19 nchini na mwenendo wa ugonjwa huo duniani, serikali inalegeza masharti kwa wasafiri wanaoingia nchini ambao wamekamilisha dozi ya chanjo ya UVIKO-19.

"Hivyo kuanzia Machi 17, 2022 wanaondolewa hitaji la kuwa na cheti cha kipimo cha kuthibitisha kutokuwa na maambukizi (negative RT - PCR certificate) kilichokuwa kikihitajika hapo awali,"anasema Ummy.

Waziri huyo anataja masharti hayo na mengine akiahidi wiki mbili zilizopita kuwapo kwenye mwongozo wa wasafiri ambao utakuwa ukibadilika kulingana na mwenendo wa maambukizi ya ugonjwa huo nchini na duniani kwa ujumla.

Pia, serikali inaongeza wigo wa uchunguzi wa maabara katika mikoa yote nchini, kuhakikisha upatikanaji wa majibu ya wagonjwa kwa wakati; huduma za kipimo cha haraka (COVID-19 Rapid Antigen Test) kuanza kutolewa ndani ya wiki moja katika vituo vya huduma za afya nchini.

Pia, anasema takwimu zinaonyesha zaidi ya asilimia 90 ya wagonjwa wanaolazwa na wanaohitaji huduma za wagonjwa mahututi ni ambao hawajachanja.

Sambamba na chanjo anahimiza wananchi kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa huo.

"Narudia kusisitiza kuwa UVIKO-19 bado upo na hutokea kwa mtindo wa mawimbi yanayoambatana na mabadiliko mbalimbali," anaeleza.

Pia, anataja mwelekeo sasa ni kuendelea kutoa huduma za kudhibiti UVIKO-19 kupitia huduma nyingine jumuishi za afya kama vile kifua kikuu, huduma za mama na mtoto, huduma za VVU/UKIMWI, huduma za malaria, huduma za magonjwa yasiyoambukiza na kadhalika.

Hata hivyo, ripoti mpya ya Wizara ya Afya iliyotolewa na Mganga Mkuu, Dk. Aifello Sichalwe jana, inataja hali ya kuwapo visa vitano vya maambukizi kwa siku kutoka 138 ya Desemba mwaka jana.



Shughuli za uchanjaji kitaifa, dhidi ya ugonjwa Uviko 19, wilayani Songwe. **PICHA: MTANDAO.**

## MAZINGIRA

### ELIMU KWA WACHIMBAJI WADOGO ...

# Serikali imeamua kushughulikia shida ya utumiaji baruti na watoto migodini

- Wanaoiba kaboni za kuchimba 'kazi kwao'
- Maofisa madini kuwapitishia darasa waliko



Mkurugenzi wa ukaguzi wa Migodi na Mazingira hapa nchini Mhandis Henry Mditi akiendesha mafunzo kwa wachimbaji wa dogo wilayani Kahama juu ya usalama mahala pakazi, uendeshaji wa mitambo ya uchenjuaji na sheria za madini ambazo zimekuwa zikifanyiwa marekebisho mara kwa mara. **PICHA: SHABAN NJIA**

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**

KUSAHAULIKA kutolewa elimu juu ya usalama sehemu ya kazi katika eneo la wachimbaji wadogo wa madini, inatajwa kuchangia kutokea ajali ambazo zingeweza kuzuilika.

Wachimbaji hao wadogo wamekuwa wakishindwa kudhibiti ajali na majanga eneo lao la uchimbaji, kutokana na ufahamu mdogo, pia namna ya kujikinga maeneo yao ya kazi, baadhi wanadhurika, kupoteza ajira.

Hapo kuna matukio ya kuangukiwa udongo shimoni, hoja ikiwapo kwamba ni ambayo yangeepukwa hatua sahihi za kiusalama zingechukuliwa.

Ikirejewa tukio la mwezi Desemba, mwaka 2015, wachimbaji wadogo watano walifukiwa na kufa kwenye mgodi wa Nyangarata, uliopo katika Halmashauri ya Msalala.

**HATUA YA WIZARA**

Kwa kuona umuhimu wa elimu kwao, Wizara ya Nishati na Madini, kupitia Tume ya Madini, imeanzisha utaratibu wa kuwatembelea wachimbaji wadogo na kuwapatia elimu ya usalama mahali pa kazi, usimamizi wa baruti, uendeshaji mitambo ya uchenjuaji, pia sheria za madini zinazofanyiwa marekebisho kila mara.

Mhandisi Henry Mditi, Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Migodi na Mazingira nchini, anasema wameanzisha mafunzo hayo endelevu kuhakikisha wachimbaji wanafanya kazi kwa usalama wakati wote.

Pia, anasema kuna mafanikio makubwa kwenye Tume ya Madini katika usimamizi wa sheria za madini zilizopo, ikiwamo katika ukusanyaji mapato na maduhuli ya serikali kila mwaka, huku wachimbaji wote wakiwa kwenye mazingira salama.

Mhandisi Mditi anafafanua wamebaini ajali nyingi kwa wachimbaji wadogo zinasababishwa na miundombinu duni, pamoja na kutumia baruti isiyofuata utaratibu uliokusudiwa na kutunza manzigira ambayo siyo salama.

"Tusingependa kuona wachimbaji wanapata riziki zao katika mzingira ambayo siyo salama kwao na kupoteza maisha kwa kukosa ufahamu ama kutokuzingatia sheria, hivyo tunatoa elimu hii ili kuzuia majanga yasiendelee kutokea katika maeneo yao ya kazi" anasema Mhandisi Mditi.

**WACHIMBAJI WADOGO.**

Peter Chikwema, ni mchimbaji kutoka mgodi mdogo wa Nyamishiga katika Halmashauri ya Msalala analiomba Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kushiriki kuisaidia kukabili maafa katika maeneo yao ya uchimbaji.

Chikwema anasema, wao kama wachimbaji wadogo hawajapata mafunzo ya uokaji na afya kazini kutoka mamlaka husika.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wadogo mkoa wa Kimadini Kahama (SHIREMA) Joseph Nalimi, anasema wengi hawana hata uelewa wa kazi za Jeshi la Zimamoto, wakidhani ni moja tu la kuzima moto unapotokea kwenye makazi ya watu.

Analalamika kuna pengo kubwa la uelewa kati yao na watendaji wa Zimamoto anaosema wanaamini kwamba

asilimia kubwa ya ajali zinazotokea maeneo ya uchimbaji, wahusika wake wanamudu kuyadhibiti, jambo ambalo Nalimi anakataa kuwa sio sahihi.

**OFISA MADINI**

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Kimadini wa Kahama, Mhandisi Jeremiah Hango, anakubali wachimbaji wadogo wa madini wamekosa mafunzo sahihi ya kazi zao, hasa katika kipengele cha uokoaji kwenye ajali za migodini. Anasisitiza, wakaguzi katika migodi hiyo, wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kujua kazi hiyo.

Anaahidi kuwa Jeshi la Zimamto na Uokoaji Kahama, litaendesha mafunzo hayo kwa wakaguzi wa migodi ya wachimbaji wote, hivyo anawaomba wahusika kuunda kundi litakalokuwa rahisi kulifikia na kuwatafuatia wataalamu kutoka mamlaka husika.

**WATOTO NA HATARI**

Dk. Arnold Gessase, Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Tume ya Madini, anawataka wachimbaji kuacha tabia ya kuwatumikisha watoto katika shughuli za uchimbaji madini, kwani wanakiuka sheria za uchimbaji madini.

Anasema, wachimbaji wengi wamekuwa wakiwatumia watoto migodini, ikiwamo kwenye ubebaji mawe yanayosadikiwa kuwa na madhara mengine yanayohatarisha afya ya mtumiaji, ambayo ni kinyume na masharti ya leseni zao.

Dk. Gessase anaonya mchimbaji atakayebainika kuwatumia watoto wadogo katika shughuli zao, atawajibishwa kisheria, ikiendana na kunyang'anywa

leseni yake, pia kufikishwa mahakamani.

**WIZI WA KABONI**

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama Timothy Ndaya, anatangaza kiama kwa wachimbaji wadogo wanaojihusisha katika vitendo vya wizi wa kaboni zinazosadikiwa kuwa na madini ya Dhahabu hali ambayo imekuwa ikisababishia serikali kuendelea kukosa mapato yake.

Anatahadharisha: "Wilaya tumejipanga vizuri kuhakikisha wanaojihusisha na tabia ya wizi wa kaboni kutafuta kazi zingine za kufanya kabla ya kuanza kuwachukulia hatua."



Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga Timoth Ndaya akifungua mafunzo ya Usalama mahala pakazi kwa wachimbaji wadogo (hawapo pichani) yaliyokuwa yakiendeshwa na Wizara ya Madini chini ya Tume yake. **PICHA: SHABAN NJIA**





# Wizara yatoa sababu ongezeko la homa, mafua na kubanwa kifua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imebainisha kuwa kuongezeka kwa wagonjwa wenye dalili za homa, kukohoa, mafua, kubanwa kifua na maumivu ya mwili hususan watoto kwa mkoa wa Dar es Salaam kumetokana na kuwapo kiwango kikubwa cha virusi vya mafua ya 'Influenza A'.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa umma na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, Machi 22 hadi 25, mwaka huu, wizara ilituma timu ya wataalamu kwenye mkoa wa Dar es Salaam kupita katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kufuatilia magonjwa hayo ya mfumo wa njia ya hewa kwa watoto waliokuwa wamelazwa wenye umri chini ya miaka 12.

Dk. Sichalwe pia alisema katika ufuatiliaji huo sampuli 123 zilizochukuliwa kutoka kwa watoto wenye dalili hizo, matokeo yalionyesha kuwa sampuli 16, sawa na asilimia 13 zilikuwa na virusi vya Influenza A na sampuli zote hazikuwa na UVIKO- 19.

"Kiwango hiki cha asilimia 13 ni kikubwa kulinganisha na kile cha wastani wa asilimia tano hadi sita ambacho kimekuwapo hapa nchini kwa muda mrefu. Kiwango hiki inawezekana ndicho kilichosababisha ongezeko la watu hasa watoto wenye dalili tajwa katika vituo vya kutolea huduma za afya hususan katika mkoa wa Dar es Salaam," alisema.

Hali hiyo, alisema imejitokeza wakati bado kuna UVIKO-19 nchini na takwimu za matokeo ya upimaji katika kipindi Januari hadi Machi 20, mwaka huu, zimeonyesha kupungua kwa wagonjwa kutoka wastani wa 138 kwa siku Desemba, mwaka jana, hadi watano kwa siku kwa Machi, mwaka huu.

Vilevile, alisema Wizara inaendelea kufuatilia tabia za anuwai za virusi vinavyosababisha UVIKO-19 na kubaini kuwa hakuna anuwai mpya nchini zaidi ya Omicron.

"Wizara ya Afya inaendelea kuchukua hatua stahiki na inawaagiza watumishi wa afya kuimarisha ufuatiliaji wa wagonjwa wote wanaohisiwa kuwa na dalili za magonjwa yanayoathiri mfumo wa njia ya hewa," alisema.

Pia alisema wizara inaendelea kuchukua sampuli kwa wagonjwa wote wenye dalili za magonjwa yanayoathiri mfumo wa njia ya hewa.

Alihimiza kuendelea kutoa elimu ya afya kuhusiana na magonjwa yanayoathiri mfumo wa hewa kwa kutumia njia mbalimbali ikiwamo vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na vituo vya kutolea huduma.

"Wizara inatoa wito kwa watu wote wenye dalili za homa, kikohozi na mafua kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili wapate matibabu sahihi.

Pia wizara inatoa rai kwa wananchi kutotumia dawa bila kuandikiwa na wataalamu wa afya," alisema.

Alishauri wananchi kuendelea kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 katika vituo vya kutolea huduma za afya, na kukamilisha dozi ili kupata kinga kamili.

## Mifugo milioni 1.5 tu yawekewa alama

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa hadi kufikia Januari, mwaka huu, mifugo 1,500,215 sawa na asilimia tatu imevishwa hereni za utambuzi.

Dk. Gibonce Kayuni kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa wafugaji uliofanyika jijini hapa.

Alisema ng'ombe 1,219,481 sawa na asilimia tano, punda 56,309 sawa na asilimia 13, mbuzi 167,298 sawa na asilimia moja, kondoo 61,571 (asilimia moja) wamewekewa alama hizo za utambuzi.

Pia alisema lengo la serikali ifikapo Septemba, mwaka huu, ni mifugo milioni 45. 92 iwe na alama za utambuzi.

"Hadi sasa mikoa 14 imeshaanza kuweka alama za utambuzi wa mifugo mbalimbali ambayo ni Rukwa, Katavi, Tabora, Kagera, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dodoma, Morogoro, Pwani, Iringa, Songwe, Mtwara na Simiyu.

Alisema kuna mikoa iko kwenye maandalizi ya uwekaji hereni hizo ambayo ni Manyara, Kigoma, Singida, Shinyanga, Geita, Mara, Mwanza, Lindi, Ruvuma, Njombe, Dar es Salaam na Mbeya.

"Mikoa tajwa bado iko kwenye maandalizi ya kuanza ya utambuzi wa mifugo kwa njia ya hereni na wizara itaendelea kutoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa utambuzi wa mifugo kupitia hereni," alisema.

Alisema kiwango cha mifugo iliyowekwa alama za utambuzi bado ni ndogo kutokana na vikwazo mbalimbali vikiwamo ukame kwa muda mrefu uliosababisha mifugo mingi kukonda na wafugaji wengi kuhama katika maeneo yao ya asili kwa ajili ya kutafuta maji na malisho, hivyo kushindwa kufanyika utambuzi.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Kaspar Mmuya (kulia), akizungumza na wajumbe kwenye kikao cha kujadili Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), jijini Dodoma juzi. Katikati ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Balozi Dk. Pindi Chana na Naibu Waziri, Ummy Nderiananga. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Kilaini ataka mfumo usawa jinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuweka mfumo rasmi ambao utasaidia wanawake kushirikishwa katika uongozi na ngazi za uamuzi kama ilivyo kwa wanaume bila kuwapo ubaguzi au udhalilishaji wa kijinsia.

Askofu Method Kilaini kutoka Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), alitoa ombi hilo jana alipokuwa akifungua mdahalo wa kitaifa kuhusu nafasi ya viongozi wa dini katika kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye uongozi na ngazi za uamuzi ulioandaliwa na Shirika la Wanawake la Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF).

Kilaini alisema ili nchi yoyote ili ipige hatua ni lazima kuwashirikisha wanawake katika uamuzi na mipango ya kijamii kisiasa na kiuchumi.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, idadi ya wanawake nchini ni asilimia 51 ni kundi hilo kubwa halipaswi kutengwa katika nafasi za uongozi na ngazi za uamuzi.

"Ili kundi hili la wanawake kupata ushiriki wa uhakika kwenye uongozi na ngazi za maamuzi (uamuzi) lazima kuwapo na mfumo rasmi utakaosaidia kundi hili kuingia katika uongozi bila kuwapo kwa upendeleo au ubaguzi.

"Ni lazima kuwapo na sheria na sera ambayo itaelekeza kuwa kundi hili ni lazima kuwepo katika ngazi na maamuzi bila kutegemea viti maalum ili kuweza kufikia usawa wa kweli kama ambavyo hata vitabu vya dini vinaelekeza kuhusu usawa kwa wanaume na wanawake," alisema.

Pia alisema utafiti unaonyesha kuwa iko sababu ya kuwapo kwa sheria mahsusi itakayosimamia suala hilo ili kuleta uwiano mzuri katika nafasi mbalimbali za uongozi nchini."Katika nafasi za uongozi kama vile wenyeviti wa mitaa, madiwani bado ziko chini lakini hata katika ubunge idadi bado iko chini sana pamoja na uwapo wa viti maalum," alisema Askofu Kilaini.

Naye Mratibu wa WiLDAF, Anna Kulaya, alisema lengo la mdahalo huo ni kujadiliana na viongozi wa dini mchango wao katika kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye uongozi na ngazi za uamuzi.

Kulaya alisema viongozi wa dini wanayo nafasi kubwa ya kuelimisha jamii kutambua umuhimu wa ushirikishwaji wa kundi la wanawake katika uongozi na ngazi za uamuzi.

"Ipo haja ya kuwapo kwa mfumo rasmi ambao utawezesha wanawake kushiriki katika uongozi na ngazi za maamuzi badala ya kuendelea kutegemea viti maalum ambavyo navyo vinawanyima kuwa na fedha za mfuko wa jimbo, nilazima tuwe na mfumo ili jinsia zote mbili kushiriki katika ngazi za maamuzi," alisema Kulaya.

Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustafa Rajabu, alisema ushiriki katika nafasi za uongozi na ngazi za uaamuzi kwa wanawake ni jambo muhimu kwa kuwa Mungu aliumba watu wote katika usawa.

"Vitabu vya dini vinaonyesha pia mwanamume na mwanamke Mungu amewaumba katika usawa. Lazima tuwape wanawake nafasi za uamuzi ili waje na mtazamo wa tofauti na wanaume ili tupate ladha zote mbili," alisema.



# RC ataka watoto wenye ulemavu kujengewa miundombinu rafiki

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewaomba wadau wa elimu mkoani humo, kuendelea kujenga miundombinu rafiki kwa watoto wenye ulemavu ili waweze kusoma kwa utulivu na kutimiza ndoto zao.

Homera alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu mwitikio wa wadau wa elimu katika kuisaidia serikali kujenga miundombinu ya shule kwa ajili ya watoto wenye ulemavu.

Alisema licha ya serikali kusaidia ujenzi wa vyumba vya madarasa na samani ni muhimu pia wadau wakaendelea kuunga mkono jitihada hizo kwa kusaidia vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ujenzi wa viwanja vya michezo ili watoto wenye ulemavu wafurahie wanapokuwa shuleni.

"Serikali imetusaidia mno kuboresha miundombinu ya shule zetu wazazi wamepunguziwa mzigo wa michango, ni wakati sasa kwa wadau kusaidia mambo mengine kama vile kutupatia vifaa vya kujifunzia na kufundishia watoto wenye ulemavu ambayo itasaidia watoto kujifunza kwa vitendo zaidi na kuongeza uelewa wa mambo," alisema Homera.

Vile vile, katika kuonyesha nia ya kuboresha mazingira ya watoto wenye ulemavu, serikali ya mkoa iko mbioni kujenga shule za kisasa kwa watoto wenye ulemavu ambazo zitakuwa na miundombinu rafiki ya kujisomea.

Alisema shule hizo zitakuwa za mfano nchini na kwamba serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali watakamilisha ujenzi huo.

"Tumeona vikwazo mbalimbali wanavyokabiliana navyo watoto wenye ulemavu ikiwamo madarasa na miundombinu mingine ya kujisomea watoto hao sasa ujenzi wa shule mbili msingi na sekondari utakuwa mwarobaini wa kutatua shida hiyo," alisema Homera.

Kwa upande wake, Ofisa Taaluma Mkoa wa Mbeya, Wilbroad Yanga, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Alisema shule ya msingi yenye mahitaji maalumu ya Katumba II iliyoko wilayani Rungwe, imetengewe Sh. milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa bweni, milioni 90 ujenzi wa jengo la utawala pamoja na vyumba vitatu vya madarasa lengo likiwa ni kupunguza msongamano wa watoto shuleni hapo.

Alisema Shule ya Msingi Katumba II inakabiliwa na tatizo kubwa la miundombinu ya madarasa kutokana na mrundikano wa wanafunzi ambao wanatoka maeneo mbalimbali nchini.



Mkurugenzi wa Shirika la Child Support Tanzania, Noela Msuya, akimfanyia mazoezi mtoto mwenye ulemavu wa viungo vya mwili, Davis Mwasajone ambaye anasoma darasa la awali katika shule inayomilikiwa na shirika hilo, Iwambi, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mvua za wastani zasaidia maharagwe kustawi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KIASI cha wastani wa mvua za masika zinazoendelea kunyesha mkoani Mbeya, kimesaidia hali zao la maharagwe shambani kuendelea kustawi vizuri ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, matokeo hayo ni jitihada za watafiti wa mazao ya chakula na biashara kutoka kituo hicho ambao wamejikita kuwasaidia wakulima kwa kuwapatia ushauri namna bora ya kulima zao hilo.

Dk. Bucheyeki alisema pia TARI waliwapatia wakulima mbegu bora za maharagwe ambayo inahimili mabadiliko ya tabia nchi ikiwamo mvua nyingi.

"Tunafurahi kuona zao la maharagwe shambani linaendelea kustawi vizuri tumetembelea mashamba kadhaa na kujionea hali halisi, tunatumaini mwaka huu mavuno yatakuwa mengi kwa sababu tuliwashauri kutumia mbegu bora tulizozifanyia tafiti sisi kituo cha Uyole," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema uamuzi huo wa kuwapatia wakulima mbegu mpya za maharagwe ulifikiwa baada ya kufanyika kikao cha wadau wa kilimo kutoka mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo Mbeya, Rukwa, Songwe na Ruvuma na walikubaliana kufanya tathmini ya mbegu mpya za zao hilo na mengine ambayo yameanza kufanyiwa utafiti kabla ya kuanza kuyasambaza kwa wakulima.

"Wataalamu wamekuja na ubunifu huo wa mbegu mpya ili kuwasaidia wakulima kukabiliana na changamoto zilizopo mpango huo unalenga kuwafikia wakulima zaidi ya 3,000 nchi zima ambao watafanyiwa majaribio ya awali kabla ya kuanza kuisambazwa kwa wakulima wengine," alisema Dk. Bucheyeki.

Mtafiti wa maharagwe kutoka TARI Uyole, Catherine Mwakabungu, alisema mbegu hizo mpya za maharagwe zimebuniwa kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi na kwamba sasa wanafurahi kuona mazao mengi shambani.

Alisema mbegu hizi zitaweza kuhimili hali ya hewa mahali popote na kwamba kila mwaka wakulima 1,000 watanufaika na mbegu hizo ambazo alisema zina mavuno mengi.

Miongoni mwa wadau wa uzalishaji mbegu mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Fadhili Kasubiri, alisema mbegu hizo zimekuja wakati muafaka na zitawasaidia wakulima kujikwamua na umaskini kwa kupata mavuno mengi.

Msindikaji wa mazao, kutoka eneo la Ikowo mkoani Rukwa, Remi Mariva, alisema kwa kipindi kirefu wamepata mavuno kidogo kutokana na aina ya mbegu wanazozitumia.

Alisema anaamini mbegu hizo mpya zitasaidia kupata mavuno mengi na kurahisisha shughuli za kusindika mazao.

## Songwe yaimarisha uhusiano kibiashara na Zambia

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

SERIKALI ya Mkoa wa Songwe, imesema katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, mkoa huo umeimarisha diplomasia na kuweka mazingira mazuri ya kibiashara baina yao na nchi jirani ya Zambia kupitia mpaka wa Tunduma.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, wakati wa kikao chake na wanahabari wa mkoa huo ambapo alisema wanajivunia kuona kuna ushirikiano mzuri wa kibiashara baina ya Tanzania na Zambia.

Alisema wameondoa baadhi ya tozo kwa wafanyabiashara wanaosafirisha bidhaa zao kupitia mpaka wa Tunduma na kufungua milango ya uwekezaji na biashara baina ya Watanzania na Wazambia kupitia mpaka wa Tunduma.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan wakati anaingia madarakani aliwaeleza Watanzania vipaumbele vyake kuwa ni kuimarisha usalama wa taifa, kukuza ushirikiano wa kidiplomasia na nchi nyingine pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Kutokana na mikakati hiyo Mkoa kwa Songwe unajivunia kushika nafasi ya pili kitaifa katika ukusanyaji wa mapato nchini na mji wa Tunduma ndiyo umechangia kwa kiasi kikubwa mkoa huo kufanya vizuri.

"Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), walipangiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 80, lakini hadi kufikia julai 2021 tulivuka lengo la ukusanyaji huo na kufikia Sh. bilioni 92 ambayo ni sawa na asilimia 115.3 ambalo ni lengo la mwaka," alisema Mgumba.

"Kuanzia Julai 2021 hadi Februari 2022, TRA Mkoa wa Songwe, walipangiwa kukusanya asilimia 67 ya mapato, lakini mkoa umefanikiwa kukusanya asilimia 74, sawa na asilimia 111 ya lengo la miezi miezi nane na kuufanya mkoa wetu wa kushika nafasi ya pili kwa ukusanyaji mapato huku Mkoa wa Mara ukiwa kinara," aliongeza Mgumba.

Alisema hayo ni matunda ya uimarishaji wa diplomasia baina ya Tanzania na mataifa mengine yaliyoko ukanda wa nchi zilizoko Kusini mwa Afrika (SADC) zikiwamo Malawi na Zambia na viongozi wa nchi hizo hufanya vikao vya ujirani mwema.

"Mpaka wa Tunduma unapitisha zaidi ya asilimia 65 ya mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam, kuboreshwa kwa ushirikiano miongoni mwa nchi za SADC kumesaidia wafanyabiashara kufanya kazi zao kwa uhuru.

Akizungumzia mafanikio hayo, Kaimu Ofisa Forodha Mfawidhi wa mizigo ya mafuta, Kituo cha Forodha Tunduma, Yusto Siwiti, alisema kutokana na ushirikiano mzuri na mazingira mazuri yaliyotengenezwa na serikali makusanyo yameongezeka kwa kiasi kikubwa katika mpaka wa Tunduma ambao unaunganisha nchi ya Tanzania na Zambia.





# TPSF yawanoa wajasiriamali Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kupitia mradi wa kuchipuza ukasimishaji haki za biashara, umewafunda wajasiriamali Zanzibar ili kuzalisha biashara zao na kuwa na soko la uhakika kitaifa na kimataifa.

Akizungumza wakati akifunga mafunzo ya siku sita kwa baadhi ya wajasiriamali hao kutoka Unguja na Pemba, yaliofanyika Mjini Zanzibar kiongozi mwelekezi wa mradi huo, Wambugu Wa Gichohi, alisema mafunzo hayo yalilenga kukuza biashara katika mfumo wa pamoja ili kujulikana kimataifa.

Alisema mfumo huo unatumika sehemu nyingi duniani, lakini kwa Tanzania na Afrika dhana ya matumizi ya mfumo huo bado haijajulikana kwa wafanyabiashara jambo linalowafanya washindwe kukuza biashara zao.

Alisema mfanyabiashara mdogo hawezi kufikia soko kubwa lakini anapokuwa ameunganishwa na wengine kupitia mifumo ya kisasa ya kimtandao itamwezesha mkulima kupata soko kubwa duniani.

Alisema kuwa ukosefu wa soko la bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi na wafanyabiashara wadogo na wakati ni miongoni mwa changamoto zinazowakwamisha kukua kibiashara katika ngazi za kimataifa.

"Wafanyabiashara wengi wamekuwa wakianzisha biashara zao lakini wanashindwa kukua kwa sababu ya kukosa masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi," alisema.

Aliwataka wajasiriamali hao kuyafanyia kazi mafunzo waliyopewa na kuwa mabalozi wazuri kwa wezao ili nao wakuze biashara zao.

Muhammed Juma Haji, mfanyabiashara kutoka Kisiwani Pemba, alisema mafunzo hayo yamemsaidia kuwa wazalishaji mzuri wa bidhaa wanazotengeneza na kufanyakazi kwa ufanisi.

Alisema wamejifunza mambo mengi ikiwamo kuwa na mpango kazi wa kuendesha biashara ili kusaidia katika uendeshaji wa bidhaa wanazozalisha.

## Waziri ataka nidhamu, ushirikiano kazini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, amesema ushirikiano wa pamoja unaleta maelewano katika sehemu ya kazi na kukuza uhusiano mwema unaojenga imani na mapenzi baina yao.

Aliyasema hayo alipofanya mazungumzo na wafanyakazi wa ofisi hiyo Mjini Zanzibar na kuwasisitiza kuwa suala la nidhamu na heshima katika kazi ni jambo la msingi huku wakijua kuwa taifa linawategemea.

Waziri huyo aliwataka wafanyakazi hao kuzingatia muda wa kuingia na kutoka kazini na inapotokea hali ya dharura kutoa taarifa na si vyema kunyamaza kwa sababu kunaweza kupoteza haki zao za msingi mambo ambayo hayana tija kiutendaji.

"Hakikisheni mnajikita katika majukumu ya kazi na mmoja wenu anapoondoka majukumu hayalali bali kazi iendelee ndio maana nawasisitiza kupendana pia msifanye kazi kwa mazoea badala yake jitahidini kuleta ufanisi ili maendeleo yaweze kupatikana," alisisitiza Harusi.

Aidha aliwataka wafanyakazi kuhakikisha wanatoa huduma stahiki kwa jamii hivyo kila mfanyakazi afahamu majukumu yake pamoja na kuzingatia suala la utoaji wa huduma kwa walioko nje ya ofisi.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Omar Dadi Shajak, alisema nidhamu na ushirikiano ndio vyenye kuleta ufanisi wa taasisi jambo ambalo linasisitizwa kwa watendaji wote.

**Aidha aliwataka wafanyakazi kuhakikisha wanatoa huduma stahiki kwa jamii hivyo kila mfanyakazi afahamu majukumu yake pamoja na kuzingatia suala la utoaji wa huduma kwa walioko nje ya ofisi.**



Mwanafunzi kutoka Skuli ya Sekondari Chumbuni, Asia Abdi Mussa, akichangia mada ya maadili wakati wa utoaji wa elimu ya maadili kwa wanafunzi wa shuleni hapo, uliofanywa na Tume ya maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa wanafunzi wa Skuli mbalimbali za Wilaya Tatu za Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wasomi kujadili usalama wa chakula

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHANGAMOTO ya usalama wa chakula na lishe inayozikumba nchi za Afrika Mashariki, imewakutanisha wanafunzi 50 kutoka vyuo vikuu vitano vya Afrika Mashariki na Denmark mjini Zanzibar katika programu maalumu ya kutafuta suluhisho.

Wanafunzi hao kutoka vyuo vikuu vya Uganda, Tanzania Bara, Zanzibar na Denmark, watajadili changamoto zinazosababisha adha hiyo katika jamii na kupendekeza suluhu hasa kwenye lishe bora.

Akizungumza katika ufunguzi wa programu hiyo, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Profesa Mohamed Makame Haji, alisema kuwa mafunzo hayo ni mwendelezo wa programu iliyoanza miaka kadhaa ambayo hufanyika kwa njia ya ushindani toka vyuo vikuu hivyo.

Alisema wanafunzi hao wamegawanyika katika taaluma mbalimbali za kiafya, chakula, kilimo na elimu hivyo watajadili chakula bora ili kuondoa hali ya utapiamlo katika jamii.

"Kwa siku nne ambazo wanafunzi watakuwa hapa watapata nafasi ya kutafuta matatizo yanayowasibu wanajamii na kutumia taaluma zao uzoefu na ujuzi katika masomo ili kupendekeza majibu sahihi ya masuala mengi ya usalama wa chakula na lishe," alisema.

Naye Mratibu wa programu hiyo, Said Yunus kutoka Shule ya Elimu SUZA, alisema mpango huo unafadhiliwa na Shirika la Danida kutoka Denmark ambapo lengo ni kupanua na kupata ufumbuzi wa changamoto za masula ya lishe na chakula katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Mmoja wa washiriki, Halima Omary Mlekwa kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), alisema, baada ya programu hiyo watapata njia sahihi za ufumbuzi wa matatizo ya chakula katika jamii.

"Tunaangalia jinsi familia zinavyoweza kupata chakula na kupunguza masuala ya utapiamlo kwa hiyo tunategemea kuja na mawazo kama vijana ambayo yatakuwa na ubunifu mkubwa kutatua changamoto hizi," alisema.

Wanafunzi hao ni kutoka Chuo cha SUZA Zanzibar, Chuo cha Kilimo Tanzania (SUA), KCMC Tanzania, Gulu Uganda na Aaborg Denmark.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI

Telegramu: UHAMIAJI
Simu: 027-2751557
027-2752284
E-mail:riokilimanjaro@immigration.go.tz
Kumb. IMM/MS/DN/963
MHARIRI
MAGAZETI LA ..............

OFISI YA UHAMIAJI MKOA,
S.L.P 1049 ,
MOSHI
KILIMANJARO
Tarehe :25/03/2022

### MAOMBI YA URAIA



HII NI TAARIFA KUWA:
BW TAMIM MOHAMED SAEED MIRZA NI RAIA WA INDIA

Ambaye picha yake imeonyeshwa hapo juu,anaomba uraia wa Tanzania kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi .Yeye ni raia wa INDIA na Nchi atokayo ni INDIA. Kazi yake /Shughuli zake ni MWANAFUNZI, Anuani ya mwajiri wake/shughuli zake ni P.O.BOX 471 MOSHI. Ameishi nchini tangu 2003, Pia amewahi kuishi Mikoa/Mikoa ya ................ , Mtu yeyeto mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:

KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI,
S.L.P 512,
DAR ES SALAAM.

KNY: AFISA UHAMIAJI MKOA,
KILIMANJARO

### KUPOTEA KWA PASSPORT



**JOHN MLAWA OBOTE** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 116095** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 24/5/2019. Muda wake wa kuisha matumizi ni tarehe 23/5/2029. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/509498/2022.**

### KUPOTEA KWA VYETI



**NICHOLAUS RAYMOND MWENDA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S1045-0136** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya DAR ES SALAAM mwaka 2002 na cheti cha chuo (CERTIFICATE IN INFORMATION TECHNOLOGY) chenye namba **ADIT/00460/T.2006** mwaka 2006 na cheti cha chuo cha (ADVANCED DIPLOMA IN INFORMATION TECHNOLOGY) chenye namba **ADIT/00460/T.2006** mwaka 2009 vilivyotolewa na chuo cha INSTITUTE OF ACCOUNTANCY ARUSHA.
Polisi taarifa **DAR/URA/RB/481585/2021**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FEKON INVESTMENT.CO.LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.288 CAF** aina ya **FEKON.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake, TAARIFA YA POLISI: **KAH/RB/1947/2022.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDUGU SALOME MZIRAY STEPHANO anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T471BKU aina ya TOYOTA IST, Rangi Nyeupe. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba DOD/DOD/RB/71205/2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo WANGING'OMBE Mkoa IRINGA Usimazi wa mirathi Na 3/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MIRATHI**

**Ombi la FEDERIKA CHRISTOPHER MSIGWA Kuteuliwa msimazi wa Mirathi ya MAREHEMU MARYNSIANA CHRISTOPHER MSIGWA**

**TANGAZO**

***(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Wilaya ya Mufindi)***

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 Mwezi 03 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimazi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha wosia.
* Futa isiyohusika.

**Imetolewa leo Tarehe 02 Mwezii 03 Mwaka 2022**

.............................................
**HAKIMU**

MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBOZI
LILILOPO SONGWE
SHAURI NO.823/2021
TUMWITIKE KASHIRIRIKA....................MDAI
DHIDI YA
ADAM MTEGA......................MDAIWA

**YAH : KUITWA SHAURINI**

**KWA : ADAM MTEGA**
Fahamu kwamba **TUMWITIKE KASHIRIRIKA** amefungua shauri dhidi yako katika Baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 08/04/2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere,mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazo husu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Songwe.
Una amriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anyeruhusiwa kisheria.Ofisi za barazazipo ndani ya eneo la Vwawa-Mbozi mjini.
Kumbuka: Usipohudhuria siku hiyo Baraza litatoa amri stahiliikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04/03/2022.

..................................
T.Munzerere
MWENYEKITI
04/03/2022

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 537 LA 2021**
**SELEMANI YASSIN.........MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SOFIA KASHINDYE ...............MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**SOFIA KASHINDYE**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**SELEMANI YASSIN** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe **17/5/2022 saa 03:00 asubuhi/mchana** mbele ya **Mh R.MBILINYI** hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

**Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 29 mwezi 03/ 2022**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**MOROGORO REGISTRY**
**CIVIL APPEAL NO.14 OF 2021**
**BETWEEN**
**ELIZABETH LEONARD NYAKUNGA...........APPELLANT**
**VERSUS**
**FAUDHUL SHABANI MAVESA, ALLY RASHID MAULA, RAMADHANI SAID NGONDO................RESPONDENT**

**NOTICE OF MENTION**

**TO: ALLY RASHID MAULA, RAMADHANI SAID NGODO ..............RESPONDENT**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention 5thday of April 2022 at 09:30 A.M at the High Court of Tanzania at Morogoro.
Your required to appear in person or through your Advocate or Agents dully authorized to appear on your behalf.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time the court may proceed with the appeal for Mention in your absence.
GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 24th day of February 2022.

DEPUTY REGISTRAR
MOROGORO


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali, baada ya kupokea taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2020/2021 pamoja na taarifa ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# CAG aanza kukagua fedha wanaokubaliana na DPP

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, ameanzisha ukaguzi maalumu wa fedha na utaratibu wa kesi zilizohitimishwa kwa kufuata Sheria ya Makubaliano ya Kukiri Kosa (Pre bargain) ya mwaka 2019 ili kujiridhisha na taratibu zote na fedha zilizokusanywa.

Kichere aliyasema hayo jana alipokuwa akiwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino.

Alisema katika ukaguzi huo, ataangalia kiasi kilichokusanywa kutokana na utaratibu huo na utahusisha mali zilizotaifishwa na serikali.

**FEDHA ZA UVIKO-19**

CAG pia alisema anaendelea na ukaguzi kwenye maeneo yote yaliyopatiwa fedha za mradi wa fedha za UVIKO-19 na kuahidi kila senti ya fedha itakaguliwa kuhakikisha imefuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo husika.

"Nitakapokamilisha ukaguzi huu, nitawasilisha ripoti kwako na matokeo yake yatawekwa hadharani ili kuimarisha uwajibikaji wa fedha hizo nazingatia maelekezo uliyoyatoa wakati wa kuzindua mradi Mheshimiwa Rais," alisema.

CAG alisema alifanya ukaguzi wa fedha zilizotolewa na Benki Kuu kwa kipindi cha Januari na Machi, mwaka jana na ripoti alishakabidhi, pia ukaguzi wa miradi ya kimkakati, ukaguzi maalumu wa mifumo ya mapato na ukaguzi wa mashirika ya umma.

Alisema kwa mwaka 2020/21, amefanya ukaguzi maalumu 56. Kati yake, 37 ni za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali Kuu 12, Mashirika ya Umma sita na mmoja wa mifumo ya TEHAMA.

**MIRADI VIWANJA VYA NDEGE**

CAG Kichere alisema kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21, serikali ilitumia Sh. trilioni 1.02 kujenga na kuboresha viwanja vya ndege 12.

Alisema ukaguzi ulibaini kuwa kuna mwingiliano wa mamlaka na majukumu ya uendelezaji wa viwanja vya ndege baina ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) unaosababisha upungufu wa uwajibikaji na utekelezaji wa bajeti za miradi hiyo.

"Kuna ongezeko la gharama ya Sh. bilioni 22.35 kutokana na kutolipa fidia kaya 1,125 katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere kwa zaidi ya miaka 23," alibainisha.

Alisema kuna watu wanatakiwa kulipwa fidia lakini hawajalipwa kutokana na taratibu hazijakamilika, hivyo tangu mwaka 1997, tathmini inaonyesha deni linaongezeka kutoka Sh. bilioni saba hadi Sh. bilioni 29.

CAG pia alibaini ucheleweshaji wa malipo ya makandarasi uliosababisha tozo za riba ya Sh. bilioni 14.14 ambapo Sh. bilioni 11.39 za Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na Sh. bilioni 2.75 za Kiwanja cha Ndege cha Mwanza.

## ... Abaini shida kwenye PSSSF, NSSF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini kuna shida kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii ikiwamo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta ya Umma (PSSSF) ambao kwa miaka mitatu mfululizo, mafao ya pensheni yalizidi mapato yanayotokana na michango.

Kichere aliyasema hayo jana alipokuwa akiwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino.

Alisema pamoja na Serikali kuongeza uwezo wa mfuko wa PSSSF hadi kufikia asilimia 30, bado kiwango hicho kiko chini ya asilimia 40 inayopendekezwa.

"Mifuko ya hifadhi ya jamii ina changamoto mbalimbali kwa miaka mitatu mfululizo, mafao ya pensheni ya mfuko wa hifadhi ya jamii kwa sekta ya umma yalizidi mapato yanayotokana na michango kwa mwaka husika," alisema.

Alisema mwaka wa fedha 2020/21 mafao yalizidi kwa Sh. bilioni 767, mwaka 2019/20 yalizidi kwa Sh. bilioni 232 na 2018/19 yalizidi kwa Sh. bilioni 307.

"Hadi kufikia Juni 30, mwaka 2021 mfuko huu ulikuwa na madeni ya Sh. bilioni 323.98 kutoka kwa taasisi za serikali na mashirika mengine," alisema.

Kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii wa Sekta Binafsi (NSSF) alisema ulitoa mikopo ya Sh. trilioni 1.17 kwa taasisi 10 za serikali ambayo haijalipwa tangu mwaka 2007.

Alisema deni la serikali limeongezeka kutoka Sh. trilioni 56.76 mwaka uliopita hadi kufikia Sh. trilioni 64.52 kufikia Juni 30, 2021.

Alisema hivyo kuna ongezeko la Sh. trilioni 7.76 sawa na asilimia 13.7.

Hata hivyo, alisema kipimo cha deni la serikali kinachotumia pato la Taifa, kinaonyesha deni hilo bado himilivu.

Alisema katika ukaguzi wa benki zinazomilikiwa na serikali alibaini kiwango cha mikopo chechefu kwa Benki ya Maendeleo (TIB) kiliongezeka kutoka asilimia 41.5 mwaka 2019 hadi asilimia 51.5 mwaka 2020 kinyume na lengo la Benki Kuu ya Tanzania(BoT) cha kufikia asilimia tano.

Alisema kiwango cha mikopo chechefu kwa Benki ya TCB (Benki ya Biashara Tanzania) kiliongezeka kutoka asilimia 5.87 mwaka 2019 hadi asilimia 15.1 mwaka 2020 kinyume na lengo la BoT.

# Urasimu bandarini wamulikwa

**Na Christina Mwakangale**

UCHELEWESHAJI wa uondoaji mizigo katika bandari ya Dar es Salaam umelalamikiwa kuwa chanzo cha urasimu, hivyo kusababisha ongezeko la bei na hasara kwa wafanyabiashara, imeelezwa.

Rais Samia Suluhu Hassan alisema jana kuwa kumekuwa na malalamiko hayo kutokana na kuongezeka kwa muda wa kuondoa mizigo hadi kufikia siku 28 kutoka siku tatu au nne za awali.

Alisema malalamiko hayo yalikuwa yakielekezwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

"Namshukuru Katibu Mkuu Kiongozi amefanya 'study' ndogo lakini nzuri iliyobainisha kwamba kwa upande wa TPA, meli zinakaa siku mbili hadi tatu, lakini kwa upande wa TICTS (Kitengo cha makontena) meli zinakaa hadi siku 28. Wale wa sekta mkaangalie kuna nini huko TICTS.

"Hawa ni kampuni binafsi, lakini waendane na masharti na taratibu zilizowekwa na bandari. Hatujui kuna ajenda gani, kuweka meli siku 28 na kutokana na malalamiko yanayosemwa meli nyingine zinaondoka bila kushushwa mizigo.

"TPA wanakwambia meli zote zilishusha mizigo kwa tarehe hizi. Meli ambazo zinaondoka bila kushusha mizigo ni za TICTS," alisema Rais Samia.

**UKAGUZI MAGARI**

Rais alimwagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kushughulikia suala hilo ikiwamo ucheleweshaji wa kushusha mizigo hususan magari.

"Eneo lile ni la kushushia magari na si la kufanyia ukaguzi, yakishushwa yanakaa pale hadi yafanyiwe ukaguzi ndio yaondoke, meli nyingine inasubiri eneo lipatikane ishushe. Tanzania hatutengenezi magari, magari yote yanatengenezwa tunakoyagiza.

"Kwa nini tusiwe na agency (wakala) eneo ambako yanatengenezwa na sio hiyo kazi ya ukaguzi kufanyika hapa, na hata ukilikagua hapa, umelitengeneza wewe, wakaguzi tusijitengenezee kazi ambazo zinaleta urasimu. Magari yakaguliwe huko mtu aje na 'certificate' (cheti), alisema.

Rais Samia, alisema ukaguzi wa magari ukifanywa kwa uadilifu nje, utaondoa urasimu.

# TUZO WANAWAKE VIONGOZI AFRIKA, BOSI DSTV ANG'ARA

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Wanawake katika Uongozi Afrika (Women in Management Africa -WIMA) , kwa ushirikiano na UNDP, European Business Group, NBC na washirika wengine wameungana kuwatunuku viongozi bora 50 wa kike wanaofanya kazi nzuri katika nyanja mbalimbali za usimamizi barani Afrika.

Huu ni mwaka wa tatu kwa WIMA na washirika wake kuandaa tuzo hizo kwa kuwaenzi viongozi hao wakuu wanawake barani Afrika ambao wamefanya vizuri katika taaluma zao, biashara na maisha ya kila siku huku wakiwatia moyo wengine ambapo mwaka 2019 na 2021, waliwatunuku zaidi ya wanawake 85 kwa utendakazi bora katika uongozi.

Tukio hili mashuhuri lililofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, pia lilishuhudia Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu wa MultiChoice Tanzania, Tike Mwakitwange, akiwa miongoni mwa waliong'ara katika 50-bora sambamba na Juliana Mwapachu, Mkuu wa Masoko ya Fedha za Kigeni NBC na Juliana Temu, Mkurugenzi Mtendaji Amref Tanzania.

Aidha, lilihudhuriwa na Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Christine Musisi akiwa mgeni rasmi pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, Waziri Mkuu wa zamani wa Tanzania, Mizengo Pinda, Balozi wa Italia nchini Tanzania, Marco Lombardi pamoja na wadau wengine muhimu.

Akizungumza katika utoaji wa tuzo hizo, Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa WIMA, Naike Moshi, alisema wanawake waliotambuliwa kwenye tuzo hizo ni katika vipengele kadhaa, ambavyo ni 50-bora ya wanawake katika usimamizi Afrika, Bingwa wa Kike wa WIMA SDG, Viongozi Wanawake katika NGOs, Tuzo ya Uwezo wa WIMA, Tuzo ya WIMA Nextgen, Tuzo ya WIMA Stem, Tuzo ya He for She, Bingwa wa Chapa ya WIMA na Tuzo ya Mafanikio ya Maisha ya WIMA.

"Nimefurahi kuwaona nyote mmekusanyika hapa kwenye hafla hii ya kipekee ambapo tunaenda kuwatambua na kuwatunuku wanawake na makampuni yaliyofanya vizuri katika utendaji wao mashuhuri na bora katika kujaza pengo la kijinsia katika jamii zao kupitia kazi wanayofanya katika sekta tofauti.

"Leo ni hafla yetu ya tatu ya utoaji tuzo, na kwa mwaka huu tumeinua kiwango kwa kuitisha mkutano wa kilele wa Pan-African asubuhi. Mkutano huo ulivutia zaidi ya washiriki 300, wanaume na wanawake, kutoka ndani na nje ya nchi, ambapo tulikuwa na mijadala na midahalo mikali kuhusu mikakati ya kuvunja upendeleo unaoendana na kaulimbiu ya Siku ya Wanawake 2022," alisema na kuongeza.

"Pia tulikuwa na mijadala shirikishi kuhusu jinsi tunavyoweza kuongeza ushirikishwaji wa kifedha wa wanawake katika enzi hii ya uchumi wa kidijitali."

Akifafanua namna washindi walivyopatikana, alisema jopo la majaji liliwaelezea wanawake na wafanyabiashara walioteuliwa kwa kina, hiyo ikiwa ni baada ya kufungua dirisha la maombi kwa umma ili kuuambia ulimwengu kuhusu mafanikio yao, na baada ya kusoma wasifu wao, waliridhika kuwaorodhesha wanawake ambao wameonyesha na kufanya kazi kwa ufanisi katika nafasi zao za uongozi nchini Tanzania, Liberia, Afrika, Kusini, Msumbiji, Ghana, Nigeria, Jordan na UAE.

Aidha, Naike aliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Samia Suluhu Hassan. kutokana na kutoa fursa kwa wanawake na kuwawezesha kwa njia tofauti katika uongozi, ujasiriamali, teknolojia, na kwingineko ndani ya mwaka wake mmoja madarakani.

"Januari, wanawake walivunja dari na tuna mwanamke shupavu anayeongoza Bunge la Tanzania, Spika wetu Tulia Ackson. Rais wetu amethibitisha wazi kuwa wanawake ni nguzo imara katika kukuza maendeleo katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa," alisema Naike.



Wanawake viongozi 50-bora wakiwa na viongozi mbalimbali waalikwa wakati wa utoaji tuzo mwishoni mwa wiki, mgeni rasmi pamoja na Waziri Mkuu wa zamani wa Tanzania, Mizengo Pinda (wanne kushoto). **MPIGAPICHA WETU**

## Serikali na michuano Jumuiya ya Madola

**Na Saada Akida**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, amewataka viongozi wa vyama vya michezo kuwa wabunifu, weledi na kuonyesha ufanisi mkubwa katika mikakati yao ya kupata ushindi wakati huu wakijiandaa na michuano ya Jumuiya ya Madola.

Mashindano ya Jumuiya ya Madola yanatarajiwa kufanyika Julai hadi Agosti, mwaka huu mjini Birmingham Uingereza ambapo Tanzania imethibitisha timu zake tano kushiriki kupitia mchezo wa riadha, judo, ngumi, kuogelea na wanyanyua uzito kwa watu wenye ulemavu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu huyo, alisema viongozi wanatakiwa kuwa makini kuhakikisha timu zao zinafanya maandalizi mazuri kwa uweledi mkubwa wa kwenda kutafuta ushindi katika mashindano hayo.

Aliwataka kuandaa timu vizuri na kambi za ndani, lakini pia wafanye maandalizi yao ya kujipima nguvu katika mashindano ya ngazi ya kimataifa kabla ya kwenda katika kushiriki michuano hiyo baadaye mwaka huu.

"Ninachosema tunamalengo makubwa kuliko kipindi chochote kingine, sasa ni muda wa kuweka mikakati ya ushindi kuandaa timu kwa ubunifu na uweledi mkubwa kwa sababu tunachotaka ni kurudi na makombe tu," alisema Dk. Abbas.

Aidha, aliwaondoa hofu viongozi wa michezo shiriki na kuwaahidi kuwa watafanyia kazi mawazo, maoni na ushauri wa kujenga endapo watawasilisha mapema.

"Ikiwamo suala la makocha wa kigeni wenye viwango, kambi katika sehemu yenye hali ya hewa sawia na mashindano yatakapofanyika na hata lishe bora kwa wachezaji. Serikali haitasita kuyafanyia kazi kwa lengo la mafanikio katika michezo hiyo," alisema.

# Mchengerwa aonya sekta ya michezo

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa, amesema hatafumbia macho wala kuvumilia kiongozi yeyote atakayefanya mambo ambayo hayakubaliki ikiwamo rushwa, ubadhirifu wa fedha na upendeleo katika sekta anayoisimamia.

Mchengerwa alitoa kauli hiyo jana katika kilele cha maadhimisho ya wiki ya mafanikio ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha mwaka moja tangu aingie madarakani Machi 19, mwaka jana.

Waziri huyo alikemea vikali vitendo vya baadhi ya viongozi wa taasisi, vyama na shirikisho la michezo, kutumia nafasi walizonazo vibaya kwa kujinufaisha wenyewe au kuhujumu maendeleo ya michezo wanayoisimamia.

Alisema Rais Samia ameupiga mwingi hadi 'ameondoka nao' kutokana na kuleta mapinduzi makubwa na mafanikio katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja, hivyo akawataka wadau wote kuishi katika falsafa zake ili kuenzi kwa ufasaha maono na nia njema ya rais.

"Viongozi wenzangu niwaombe na kuwasihi sana tusimuangushe rais, bali tuunge mkono juhudi zake, nia njema na uthubutu mkubwa aliouonyesha katika kuleta mapinduzi kwenye sekta yetu na tuuenzi kwa vitendo," alisema na kuongeza:

"Kama Waziri mwenye dhamana ya michezo sitafumbia macho wala kuvumilia kiongozi yeyote kufanya mambo yasiyokubalika kurudisha nyuma juhudi za rais katika sekta ninazozisimamia kuanzia wizarani, taasisi, vyama na shirikisho la michezo."

Alisema anatambua wapo baadhi ya viongozi ambao kwa kipindi kirefu wanaendesha shughuli za vyama kwa mazoea bila kufuata taratibu wala kuheshimu na kutii mamlaka zinazosimamia michezo.

"Kwa kipindi cha uongozi wangu sitavumilia na nitamchukulia hatua kali za kisheria kiongozi ambaye atabainika kufanya matendo ya rushwa, ubadhirifu wa mali na fedha za umma, upendeleo na unyanyasaji katika michezo,"alisema Mchengerwa.

Alisema kwa mwaka mmoja wa Rais Samia, kumekuwa na mafanikio makubwa ikiwamo ongezeko la bajeti, uanzishwaji wa mfuko wa maendeleo ya michezo, ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya michezo kupitia upya utekelezaji wa sera ya michezo ya mwaka 1995.

"Kuanzisha programu ya kuibua vipaji vya michezo , ukarabati wa Uwanja wa Ndani wa Benjamini Mkapa, kutoa nafuu ya kodi katika uingizaji wa nyasi bandia, kukamilika kwa uteuzi wa shule 56 maalum za michezo nchini na ujezi wa Kituo cha Maendelezo ya Michezo katika cha Michezo Malya," alisema Mchengerwa.

Wakati huo huo Mchengerwa amemthibitisha Neema Msitha kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Bi. Consolata Mushi kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Riziki Juma Majala kuwa Msajili wa Vyama vya Michezo nchini.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WERNER KUONDOKA CHELSEA
MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Timo Werner, anataka kuondoka Chelsea na 'Blues' hao hawatamzuia nyota huyo mwenye miaka 26 ikiwa timu zitafika bei yake ya pauni milioni 33. ***(Sport1)***

### HAG KUMSAJILI ANTONY
KAMA Erik ten Hag atakuwa kocha wa Manchester United, atamsajili winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 22, kutoka klabu yake ya sasa ya Ajax. ***(Telegraph)***

### POGBA KUPUNGUZA MSHAHARA
KIUNGO wa Man United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, itabidi apunguze mshahara wake kwa kiwango kikubwa kama anataka kurejea Juventus msimu huu. ***(Calciomercato - via Mail)***

### NUNEZ KURUHUSIWA KUSEPA
MSHAMBULIAJI wa Benfica, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, anayewaniwa na Tottenham, ataruhusiwa kuondoka kama dili la pauni milioni 67 litafikiwa msimu huu. ***(O Jogo - via Sport Witness)***

### SINISTERRA ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal imeweka mezani ofa ya kumnunua winga wa Feyenoord na Colombia, Luis Sinisterra mwenye umri wa miaka 22. ***(Corriere dello Sport)***

### BELLINGHAM AWINDWA MADRID
REAL Madrid wanamlenga kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kuhusishwa na uhamisho wa Liverpool. ***(Bild)***

### ERIKSEN KUFUNGWA ZAIDI
KLABU ya Brentford inataka kurefusha mkataba wa miezi sita wa kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 30, uliosainiwa na klabu hiyo. ***(Times)***

### RAPHINHA NA BARCELONA
BARCELONA hawajawasilisha ofa ya kumnunua mshambuliaji wa Leeds, Raphinha, lakini makubaliano binafsi yamejadiliwa na wakala wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 25. Winga huyo raia wa Brazil ana kifungu katika mkataba wake kinachoamua bei yake ikiwa klabu yake itashushwa daraja. ***(Fabrizio Romano)***

### TRAORE KUBAKI CAMP NOU
BARCELONA wanamatumaini ya kumsajili tena kwa mkopo winga wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26, kutoka Wolve. ***(RAC 1 - via Goal)***

### GRIEZMANN KUONGEZEWA
KLABU ya Atletico Madrid huenda wakarefusha mkataba wa mkopo wa mshambuliaji, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 31, kutoka Barcelona, lakini hawako tayari kumwachia mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 22 ajiunge na miamba hao wa Hispania. ***(Goal)***

### WILLIAMS AIGOMEA UNITED
MLINZI wa Manchester United mwenye umri wa miaka 21, Brandon Williams - ambaye kwa sasa yuko Norwich kwa mkopo, amesema "hakuna haja" ya yeye kurudi Old Trafford kama mchezaji wa ziada. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GHANA, CAMEROON, SENEGAL RASMI KOMBE LA DUNIA 2022

●●●Lewandowski na Fernandes nao wazipa tiketi ya Qatar timu zao za Poland na Ureno huku...

**CAIRO, Misri**

TIMU za Cameroon, Ghana, Morocco, Senegal na Tunisia zimefuzu kutoka Ukanda wa Afrika kucheza fainali za Kombe la Dunia zitakazopigwa baadaye mwaka huu huko Qatar, baada ya matokeo yao ya michezo ya juzi usiku.

Cameroon ilishinda ugenini mabao 2-1 dhidi ya Algeria kwa bao la jioni na kufuzu baada ya mchezo wa kwanza Algeria kushinda ugenini 1-0.

Ghana ikaiondosha Nigeria baada ya sare ya bao 1-1 ugenini, mchezo wa kwanza uliopigwa Ghana, timu hizo zilienda sare tasa.

Morocco ikaitandika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, DRC mabao 4-1 pale Casablanca na kuiondosha kwa jumla ya mabao 5-2 baada ya awali ugenini mjini Kinshasa kutoka sare ya bao 1-1.

Sadio Mane akafunga penalti ya ushindi kwa Senegal ikiiondosha kwa matuta Misri baada ya kulingana kwa mabao, kila mmoja akishinda kwake kwa bao 1-0.

Baada ya sare ya nyumbani ya bila kufungana, Tunisia imesonga mbele kwa bao la ugenini ililolipata kwenye mchezo wa awali dhidi ya Mali.

ULAYA

Barani Ulaya, Poland na Ureno zimefanikiwa kufuzu baada ya kushinda michezo yao ya juzi usiku.

Shujaa wa Ureno alikuwa Bruno Fernandes, kiungo wa Manchester United aliyefunga mabao mawili, wakati wakiifunga Macedonia Kaskazini 2-0.

Poland ikafuzu kwenda Qatar kwa mabao ya Robert Lewandowski na Piotr Zielinski kuwapa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Sweden.

Nchi zingine zilizofuzu kutoka bara la Ulaya ni pamoja na Ubelgiji, Ufaransa, England, Serbia, Uholanzi, Hispania, Croatia na Uswisi.

AMERIKA KUSINI, KATI NA KASKAZINI

Canada ilikuwa nchi ya kwanza kufuzu kucheza Kombe la Dunia kutoka ukanda huo.

Brazil, Argentina, Ecuador, Uruguay nazo zimefuzu. Brazil ikikamilisha ratiba alfajiri ya jana kwa kuizaba 4-0 Bolivia, Argentina ikaenda sare ya 1-1 na Ecuador, Chile ikalala 2-0 dhidi ya Uruguay.

ASIA

Qatar yenyewe imefuzu moja kwa moja kutokana na kuwa mwenyeji wa mashindano hayo ikiungana na Korea Kusini, Iran, Japan na Saudi Arabia.

Iran jana imeichapa Lebanon 2-0, Syria na Iraq zikaenda sare ya 1-1 huku UAE ikiilaza Korea Kusini kwa bao 1-0.

Fainali ya mashindano hayo zitakazoshirikisha mataifa 32 zinatarajiwa kupigwa Desemba 18, 2022.

Haya yatakuwa mashindano ya kwanza kufanyika Mashariki ya Kati na yakiwa ya mwisho yakayotumia mfumo wa sasa wa kushirikisha timu 32, kabla ya kuanza kwa mfumo mpya utakaoshirikisha timu 48 kuanzia fainali za mwaka 2026.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,089

MECHI KALI
PUERTO QUITO
VERSUS
MANTA
1 | 3.25
X | 2.87
2 | 2.25

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MANCINI KUENDELEA KUINOA ITALIA



**ROME, Italia**

ROBERTO Mancini ataendelea kuinoa Timu ya Taifa ya Italia licha ya kushindwa kufuzu mashindano ya Kombe la Dunia kwa mara ya pili mfululizo ya kwanza ikiwa nchini Urusi 2018 na mwaka huu nchini Qatar.

Mancini aliiongoza timu ya Taifa ya Italia kuchukua ubingwa wa Ulaya miezi nane iliyopita, lakini amepoteza kwenye mchujo wa kutafuta nafasi kushiriki michuano ya Kome la Dunia nchini Qatar dhidi ya Macedonia Kaskazini.

Kocha Gian Piero Ventura alionyeshwa milango ya kutokea baada ya kushindwa kufuzu Kombe la Dunia nchini Urusi mwaka 2018, ambapo Ufaransa ndiyo iliyokuwa bingwa wa michuano hiyo.

Ingawa chama cha soka nchini Italia kipindi hiki kimeamua kubaki na Mancini, ambaye alirudisha hamasa kwenye timu na kuiongoza kuchukua ubingwa wa Euro 2020, kocha huyo mwenye miaka 57 bado anamkataba na shirikisho hilo ambao utaisha Mei 2026.

"Tunahitaji kuanza upya, nimezungumza na rais wa shirikisho, tumekubaliana kwenye kila kitu ambacho tumezungumza na nini tuboreshe,"alisema Mancini.

"Bado kijana na nilihitaji kushinda Euro na Kombe la Dunia, itabidi tusubiri kwa muda kidogo.

"Naipenda hii kazi na najua tukiungana na wachezaji tunaweza fanya kitu bora kingine, ukiachana na matokeo mabovu kila kitu kinaendea vizuri.

# Rio: Sioni Ronaldo akiondoka United

**MANCHESTER, England**

MCHEZAJI wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand, amesema haoni mchezaji mwenzake wa zamani, Cristiano Ronaldo akiondoka kwenye klabu hiyo kipindi cha majira ya joto hata kama watashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Ferdinand amecheza pamoja na Ronaldo pale Man United kuanzia mwaka 2003 hadi 2009, ambapo walikuwa chini ya kocha Sir Alex Ferguson huku wakifanikiwa kuchukua ubingwa wa Ulaya, Ligi Kuu mara tatu, FA mara moja na Kombe la Ligi mara mbili.

Ronaldo amejiunga na klabu ya Man United kipindi cha majira ya joto mwaka 2021, lakini tangu amejiunga kumekuwa na tetesi za kuwa anaweza kuondoka ikiwa tu, timu hiyo itashindwa kufuzu kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Sioni kama ataondoka, nataka kuwa mkweli, hata kama Man United wakishindwa kuingia kwenye nne bora," alisema Ferdinand.

"Nafikiri Ronaldo anapaswa kushughulika na Man Utd kwa mwaka mwingine. Ndio anataka kushindana, anayo hiyo hamasa ya kutaka kushinda mataji, alishazoea kufanya hivyo, amezoea kushinda tu.

"Lakini mara zote haiwezi kuwa hivyo, amekuwa na misimu mizuri karibia miaka yake yote."



## HABARI MICHEZO

9,062,840

# MAYELE AMPA PRESHA LUSAJO

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

STRAIKA wa Namungo na Timu ya Taifa, Taifa Stars, Reliants Lusajo amesema kushindanishwa na Fiston Mayele wa Yanga kumesababisha awe na presha kubwa, huku baadhi ya mashabiki wakitarajia makubwa kutoka kwake wakati lengo lake ni kuisaidia timu yake na si kushindana na mtu.

Lusajo ambaye ana mabao 10 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, sawa na Mayele, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, amesema kuwa kutokana na Mayele kuwa anafunga, basi baadhi ya mashabiki wamekuwa wakimshinikiza afunge au kufanya makubwa zaidi, kitu ambacho hakikuwahi kumtokea huko nyuma.

"Unajua mimi sishindani na mtu kwa sababu lengo si kushindana, mimi nafunga mabao kwa ajili ya kuisaidia timu yangu na misimu yote hii nimekuwa nafunga, lakini msimu huu watu wamenifanya niwe na presha ili kushindana na Mayele, mimi kufunga ni kawaida yangu na wala silali na kuwaza kuwa nakwenda kufunga au najiandaa sana, hapana, unajua vitu vingine ni asili tu, kwa hiyo sina wasiwasi nitafunga sana, ila si kushindana na mtu," alisema Lusajo.



Kuhusu Mayele anasema kuwa anamheshimu sana straika huyo, kwa sababu naye pia ametokea kumheshimu, hivyo wote wawili wanaheshimiana.

"Mayele ni straika mzuri sana na tunaheshimiana sana, lakini mimi pia nawaheshimu mastraika wengine kama George Mpole, John Bocco na Meddie Kagere. Unajua Bocco na Kagere lazima uwape heshima ya pekee kwa sababu wamefanya vitu vikubwa kwenye ligi yetu na nje ya nchi ambavyo sisi wenyewe bado hatujavifanya," alisema.

Akizungumzia Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu Bara, alisema hafikirii sana hilo, lakini pia akaongeza mchezaji yeyote si lazima wao, anaweza kuwa mfungaji bora.

"Huu ni mpira bwana, unaweza kuongoza, ukapata majeraha, ukakaa nje, wakaja wengine wanafunga wakawa wafungaji bora," alisema Lusajo ambaye amewahi pia kuichezea KMC.

Aidha, Lusajo alisema siri kubwa ya mafanikio yake katika kufunga ni kumsikiliza kocha wake kwa makini nje na ndani ya uwanja.

"Kinachonifanya nifanye vizuri ni kule kumsikiliza kocha wangu kwa makini pamoja na kushirikiana na wachezaji wenzangu," alisema Lusajo.

# Yanga Princess yatamba kupata mbadala wa Aisha

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Yanga Princess, Khalifan Mbonde, amesema kuondoka kwa mshambuliaji kinara wa timu hiyo, Aisha Masaka, hakujaacha pengo ndani ya kikosi chao na kwamba anaamini wataendelea kufanya vizuri katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Kauli hiyo ya Mbonde imekuja baada ya jana kikosi chao kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Alliance Girls katika mechi ya ligi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema kuondoka kwa mfungaji wao huyo, Aisha kwenda kucheza soka la kulipwa Klabu ya BK Hacken FF ya Sweden, hakujawaathiri lolote katika safu yao ya ushambuliaji.

Alisema nafasi ya nyota huyo tayari imekuwa na watu ambao wanatakiwa kuongeza umakini hasa katika nafasi wanazotengenezewa.

"Mchezo wa leo (juzi) dhidi ya Alliance Girls, tulipata nafasi lakini washambuliaji hawakuwa makini na hatimaye dakika za mwisho kupata bao 1-0, hii haina maana kwani ni kutokana na kutokuwapo kwa Aisha, bali ni safu ya ushambuliaji tu inatakiwa kuwa makini," alisema kocha huyo.

Alisema bado mipango yao ni kuhakikisha wanashinda mechi na kutafuta pointi katika michezo ya mzunguko wa pili ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Naye Kocha wa Alliance Girls, Sultan Kassim, alisema Yanga hawakuwa bora zaidi ya kutumia makosa waliyoyafanya mabeki na kipa wake kupata ushindi huo.

"Tumekubali kupoteza mechi hii, ila ukingalia makosa ya mabeki na kipa kufanya makosa na mchezaji wa Yanga kutumia nafasi hii kwa kutufunga bao 1-0 ndiyo yaliyowafanya kuondoka na pointi tatu," alisema Sultan.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Simba inaongoza kileleni ikiwa na pointi 33 zilizotokana na mechi 11, ikifuatiwa na Yanga yenye alama 23 lakini wakiwa mechi moja nyuma huku Alliance Girls ikiwa nafasi ya sita na pointi zake 15.



## JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/04/22 | 17:00 | Leeds vs Southampton | 2.36 | 3.53 | 2.83 |
| 02. 02/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 2.84 | 3.09 | 2.54 |
| 03. 02/04/22 | 19:30 | Borussia Dortmund vs RB Leipzig | 2.38 | 3.59 | 2.69 |
| 04. 03/04/22 | 14:00 | Rangers vs Celtic | 2.36 | 3.28 | 2.88 |
| 05. 03/04/22 | 15:30 | Fortuna Sittard vs Heracles Almelo | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 06. 03/04/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.56 | 2.96 | 2.96 |
| 07. 03/04/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Nantes | 2.55 | 3.05 | 2.90 |
| 08. 03/04/22 | 16:00 | Atalanta vs Napoli | 2.42 | 3.20 | 2.90 |
| 09. 03/04/22 | 16:30 | Augsburg vs VfL Wolfsburg | 2.86 | 3.26 | 2.45 |
| 10. 03/04/22 | 19:00 | Panathinaikos vs PAOK | 2.59 | 3.03 | 2.79 |
| 11. 03/04/22 | 19:30 | Granada vs Rayo Vallecano | 2.68 | 3.13 | 2.73 |
| 12. 03/04/22 | 20:00 | Moreirense vs Vitoria Guimaraes | 2.80 | 3.20 | 2.47 |
| 13. 03/04/22 | 21:45 | Juventus vs Inter | 2.70 | 3.25 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 31/03/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2317 | Zvezda 2005 Perm W vs Kubanochka Krasnodar W | 1.45 | 4.07 | 6.01 |
| 15:00 | 3776 | Zhfk Yenisey Krasnoyarsk W vs FK Rubin Kazan W | 1.86 | 3.30 | 3.84 |
| 15:00 | 3881 | Sidama Bunna SC vs Ethiopia Bunna SC | 2.45 | 2.65 | 3.19 |
| 15:15 | 2887 | Melaka vs Pib FC | 1.11 | 7.04 | 16.61 |
| 16:00 | 1036 | El Bayadh vs SC Ain Defla | 1.07 | 7.81 | 24.41 |
| 16:00 | 1489 | Persik Kediri vs Bali Utd Pusam | 6.04 | 3.51 | 1.54 |
| 16:00 | 1513 | NRB Teleghma vs Hamra Annaba | 1.59 | 3.41 | 5.65 |
| 16:00 | 1566 | MO Constantine vs USM Khenchela | 3.40 | 2.92 | 2.16 |
| 16:00 | 1734 | CA Batna vs MO Bejaia | 2.00 | 2.82 | 4.08 |
| 16:00 | 2420 | USM EL Harrach vs ZR Temouchent | 2.73 | 2.68 | 2.78 |
| 16:00 | 2475 | USM Hadjout vs MCB Oued Sly | 2.53 | 2.82 | 2.87 |
| 16:00 | 2768 | JSM Bejaia vs IRB Lakhdaria | 1.33 | 4.39 | 8.40 |
| 16:00 | 2897 | JSM Skikda vs Ain M'lila | 2.19 | 2.77 | 3.55 |
| 16:00 | 3030 | USM Bel Abbes vs CRB Ain Ouessara | 1.43 | 3.90 | 7.03 |
| 16:00 | 3400 | US Chaouia vs MC EL Eulma | 1.54 | 3.56 | 5.86 |
| 16:00 | 3628 | Skaf Khemis Miliana vs MC Saida | 2.19 | 2.78 | 3.51 |
| 16:00 | 3992 | Perak FA vs Kijang Rangers FC | 1.17 | 6.24 | 11.70 |
| 16:00 | 4053 | GC Mascara vs JSM Tiaret | 2.21 | 2.82 | 3.41 |
| 16:00 | 4378 | USM Annaba vs CA Bordj Bou Arreridj | 1.26 | 4.69 | 10.74 |
| 16:00 | 4607 | JS Bordj Menaiel vs Irb Ouargla | 1.35 | 4.18 | 8.35 |
| 16:00 | 4876 | ASM Oran vs RC Kouba | 2.76 | 2.76 | 2.66 |
| 16:30 | 4624 | Kokand 1912 vs Metallurg Bekabad | 1.97 | 3.26 | 3.51 |
| 17:00 | 1710 | CSKA Moscow W vs Ryazan Vdv W | 1.26 | 4.69 | 10.74 |
| 17:00 | 2665 | FK Rostov W vs FC Zenit Saint Petersburg W | 9.32 | 3.98 | 1.35 |
| 17:00 | 4042 | Bunyodkor vs Dinamo Samarqand | 1.38 | 4.19 | 7.21 |
| 17:00 | 5187 | Mosaset AL Bireh vs Shabab AL Amari | 2.11 | 3.35 | 3.06 |
| 17:00 | 5416 | Islami Qalqilya vs Shabab Alsamu | 3.79 | 3.45 | 1.83 |
| 17:00 | 5698 | WA Boufarik vs Ben Aknoun | 2.07 | 2.92 | 3.65 |
| 17:30 | 3157 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Maccabi Bnot Emek Hefer W | 2.27 | 3.59 | 2.62 |
| 18:00 | 3757 | Addis Ababa City FC vs Bahir Dar Kenema FC | 2.88 | 2.92 | 2.44 |
| 18:30 | 5107 | Sporting Gagnoa vs ASEC Mimosas | 5.86 | 3.03 | 1.67 |
| 19:00 | 1392 | MS Kiryat Gat W vs AS Tel Aviv University W | 1.48 | 4.30 | 5.28 |
| 19:00 | 2088 | Esbjerg vs Hobro | 2.04 | 3.40 | 3.16 |
| 19:00 | 4299 | FC Lokomotiv Moscow W vs Chertanovo Moskva W | 1.03 | 9.32 | 48.53 |
| 19:30 | 1173 | Hermanstadt vs Concordia Chiajna | 1.90 | 3.05 | 4.07 |
| 19:30 | 2698 | Hapoel Beer Sheva W vs Bnot Netanya W | 1.55 | 4.28 | 4.57 |
| 19:45 | 2173 | Wolfsburg W vs Arsenal W | 1.98 | 3.40 | 3.31 |
| 20:00 | 5636 | Thagafi Tulkarem vs Markez Balata | 2.39 | 3.12 | 2.78 |
| 21:00 | 1882 | RSV Meinerzhagen vs TSV Victoria Clarholz | 2.35 | 3.84 | 2.41 |
| 22:00 | 1029 | Lyon W vs Juventus Women | 1.13 | 6.79 | 15.53 |
| 23:30 | 1645 | CD Cortulua vs Fortaleza Ceif FC | 2.70 | 3.40 | 2.46 |
| 23:30 | 5462 | Puerto Quito vs Manta | 3.25 | 2.87 | 2.25 |

### IJUMAA - 01/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 2575 | Cdp Junior FC vs CA Bucaramanga Sa | 1.56 | 3.50 | 5.83 |
| 00:00 | 4954 | AD Carmelita vs Universidad De Costa Rica | 1.59 | 3.88 | 4.66 |
| 00:15 | 3304 | Deportivo Tachira vs Deportivo Lara | 1.97 | 3.11 | 3.70 |
| 00:30 | 5210 | Olmedo vs America | 2.26 | 2.88 | 3.22 |
| 01:00 | 1066 | Necaxa W vs Atletico San Luis W | 1.97 | 3.36 | 3.41 |
| 01:00 | 1490 | Colo Colo vs Union La Calera | 1.39 | 4.19 | 7.01 |
| 01:15 | 3523 | Academia Puerto Cabello vs Caracas FC | 3.80 | 3.31 | 1.87 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Alhamisi Machi 31, 2022

Nipashe



## Ghana, Cameroon, Senegal rasmi Kombe la Dunia 2022

KAMPENI...



Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, akizungumza na mashabiki wa timu hiyo wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Hamasa kuelekea mchezo dhidi ya US Gendarmerie Jumapili wiki hii. Uzinduzi wa kampeni hiyo ulifanyika jana katika Stendi ya Mabasi ya Magufuli Mbezi, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# PABLO ATOA AHADI MBILI GENDARMERIE

## ●●●Aungana na uongozi kuita mashabiki kwa Mkapa Jumapili, 200 kununuliwa tiketi...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI US Gendarmerie ya Niger wakitarajia kutua nchini leo tayari kwa mechi ya kuhitimisha hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco ameahidi mashabiki wao mambo mawili; kushinda na kuonyesha kandanda safi katika mchezo huo utakaopigwa Jumapili wiki hii.

Katika mchezo huo utakaopigwa saa 1:00 usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba yenye alama saba sawa na RS Berkane ya Morocco, inahitaji ushindi ili kutinga robo fainali ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa barani humu.

Katika Kundi D, ambalo linaundwa na Simba, Gendarmerie, RS Berkane, Asec Mimosas ya Ivory Coast watakaokuwa ugenini nchini Morocco Jumapili, ndio vinara wakiwa na alama tisa, hivyo sare tu inawatosha kutinga robo fainali. Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema kwa sasa hawana cha kufikiria zaidi ya mambo mawili, kushinda, lakini pia kuwapa burudani mashabiki wa Simba.

Alisema anaamini wachezaji wake watafuata kile alichowaelekeza na kuwapa furaha mashabiki, lakini la muhimu zaidi kwao ni kusaka ushindi ili kufikia malengo yao ya kufuzu robo fainali.

"Lengo la kwanza kubwa ni kuhakikisha tunashinda mchezo huo ambao ni fainali kwetu, pia kuonyesha kandada safi ya kuvutia mashabiki watakaojitokeza kutusapoti siku hiyo," alisema.

"Tunajua tunahitaji kushinda ili kuwapa furaha mashabiki, naamini watajitokeza kwa wingi, jukumu letu benchi la ufundi na wachezaji ni kuhakikisha tunawapa furaha ikiwamo kushinda mchezo huo."

Kuhusu hofu ya Simba kumkosa kiungo wao mshambuliaji, Pape Sakho, taarifa kutoka Kitengo cha Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, kinachoongozwa na Ahmed Ally, zimeeleza alipata maumivu ya mguu katika harakati za kuwania mpira mazoezini kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena, lakini kwa sasa yupo fiti na jana alitarajiwa kuendelea na mazoezi.

"Daktari amewatoa hofu mashabiki wetu, Sakho hakupata majeraha makubwa anaendelea vizuri na leo (jana atarejea mazoezini na atakuwa sehemu ya kikosi kitakachoshuka dimbani Jumapili kuikabili Us Gendarmerie," alisema Ahmed Ally.

Wakati huo huo, jana Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, alizindua kampeni ya hamasa kwa mashabiki kuelekea mchezo huo.

Katika uzinduzi huo, uliofanyika Stendi ya Mabasi ya Magufuli Mbezi, Dar es Salaam, Mangungu alisema uongozi pamoja na wachezaji wote wapo imara kuelekea kwenye mchezo huo na yeye binafsi akiahidi kununua tiketi 200 na kuzigawa kwa mashabiki ili kwenda kuisapoti timu Jumapili.

Kuhusu taarifa ya baadhi ya wachezaji wao kumaliza mikataba, Mangungu alisema: "Kuna baadhi ya watu ambao wanazungumzia kumalizika kwa mikataba ya wachezaji wetu wakidai wanataka kuwasajili kamwe hawatafanikiwa kwa sababu tunafahamu hizo ni propaganda tu," alisema.

Katika uzinduzi huo, ulihudhuriwa na matawi 26, jambo ambalo uongozi wa klabu hiyo umewataka hata kuzidi kuhamasishana kuhudhuria uwanjani siku hiyo ili kushirikiana pamoja kufanikisha ushindi kwa kuwasapoti wachezaji.

## Yanga, Azam FC zatafutiana pumzi

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikishuka dimbani jana usiku dhidi ya Mafunzo ya Zanzibar kutafutia kasi mechi yao Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, Kocha Mkuu wa 'Wanalambalamba' hao, Abdihamid Moallin, amesema tayari wamepata kipimo kizuri cha kuwavaa.

Yanga jana ilishuka katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kuvaana na Mafunzo ikiwa ni maandalizi kuelekea mechi dhidi ya Azam FC ambao nao mwishoni mwa wiki walijipima nguvu dhidi ya DTB ya Ligi ya Championship kabla ya miamba hiyo ya Ligi Kuu Bara kupepetana Aprili 6, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Moallin alisema mechi waliyocheza ya kirafiki ni muhimu sana na wamepata kipimo tosha kuelekea katika maandalizi ya mechi ijayo.

Alisema mechi dhidi ya DTB FC imempa mwanga wa kuona kikosi chake na kupima utayari wa wachezaji wake baada ya kufanya mazoezi ya wiki nzima.

**"Tumepata mchezo mzuri wa kujipima nguvu baada ya kufanya mazoezi muda mrefu, tunaendelea na maandalizi yetu kuji andaa dhidi ya Yanga, mchezo utakuwa mgumu na ushindani kwa sababu kila mmoja anahitaji pointi muhimu," alisema kocha huyo.**

Alisema anafanyia kazi mapungufu ya kikosi chake, lakini pia ubora wa wapinzani wao, Yanga kuhakikisha wanabakiza pointi nyumbani katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema michezo miwili ndani ya uwanja huo hawakupata matokeo mazuri na wanarejea kuhakikisha mechi dhidi ya Yanga wanafanikiwa kufikia malengo ya kubakiza pointi tatu nyumbani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >